





## Unyanyasaji kazini waishtua serikali, bosi ashtakiwa kwa kulazimisha ngono

UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 4, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581149

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Mwili wa askofu wakutwa ziwani



**Ni** aliyetoweka kwa siku nne. Polisi, familia... *Endelea Ukurasa. 2*




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na kuchangia mada mbalimbali katika Mkutano wa Mtandao wa Viongozi Wanawake wa Afrika, jijini Zanzibar jana. Kulia kwake ni Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde. **PICHA: IKULU**

## Samia ataja kikwazo ukombozi wanawake

UKURASA 3

## Mlinzi aliyedaiwa kuuawa na bosi aokotwa msituni

UK 2

**MICHEZO** **MAYELE HATIHATI KUIKABILI PRISONS** UK. 24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughle, akiwasaidia mafundi wa kampuni ya Road Sky, kuchora alama za kivuko cha waenda kwa miguu katika Barabara ya Sokoine, jijini Dar es Salaam, alipokuwa katika ziara ya kukagua shughuli za maendeleo katani kwake, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwili wa askofu wakutwa ukielea ziwani

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Victoria Nyanza, Boniface Kwangu (58), amefariki dunia huku mwili wake ukikutwa unaelea katika Ziwa Victoria baada ya kupotea kwa siku nne.

Askofu Kwangu, mkazi wa Sibula wilaya ya Ilemela, anadaiwa kuwa aliaga nyumbani kwake Novemba 28, mwaka huu, majira ya asubuhi kuwa anakwenda Sengerema kupokea malipo yake ya mwisho ya Sh. milioni 2.5 zilizotokana na mauzo ya kiwanja chake pamoja na nyumba yake kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Inadaiwa kuwa baada ya kufika huko, hakufanikiwa kupewa fedha hizo kutokana na kilichoelezwa kuwa hakuwa na nyaraka za umiliki wa eneo hilo ndipo akaamuliwa kurudi Mwanza ili kuchukua nyaraka hizo na kuzipeleka ili amaliziwe malipo hayo.

Hakurejea nyumbani mpaka ilipofika jioni ya siku hiyo na familia ikapata wasiwasi aliko kwa kuwa alikuwa hapatikani pia kwenye simu yake ya mkononi.

Hatua hiyo ilisababisha familia kwa kushirikiana na uongozi wa kanisa kutoa taarifa Kituo cha Polisi Kirumba, jijini Mwanza pamoja na kuzungukia katika vyombo vya habari ili kusambaza taarifa hizo bila mafanikio.

Akithibitisha kupatikana kwa mwili wa Askofu huyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Willbroad Mutafungwa, alisema juzi majira ya asubuhi kwa kushirikiana na wananchi, waliupata mwili wake ukiwa unaelea katika Ziwa Victoria, wilaya ya Misungwi na kisha kuuopoa.

Kamanda Mutafungwa alifafanua kuwa mwili wa Askofu Mstaafu Kwangu ulikuwa ndani ya maji karibu na eneo la daraja la Dr. John Pombe Magufuli, Kigongo - Busisi.

"Baada ya kupokea taarifa ya kupotea kwa Askofu Mstaafu Kwangu, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na familia na watu mbalimbali, tulianza kufanya ufuatiliaji ili kubaini alipo.

"Wakati uchunguzi ukiendelea, zilipatikana taarifa kutoka kwa wananchi wema kwamba katika kijiji cha Kigongo, kata ya Idetemya Wilaya ya Misungwi ndani ya maji katika Ziwa Victoria jirani na daraja la Dr. John Pombe Magufuli umeonekena mwili wa mtu wa jinsia ya kiume ukiwa unaelea majini," alisema Mutafungwa. Alisema polisi walifika eneo hilo na kwa kushirikiana na wananchi, waliopoa mwili huo na kutambulika kuwa ni wa Askofu Kwangu kisha kuuchukua na kuuhifadhi hospitalini kwa hatua zaidi za kiuchunguzi kabla ya kukabidhiwa kwa ndugu na kanisa kwa ajili ya mazishi.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mutafungwa alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi, hivyo kuiomba familia, ndugu, jamaa na wananchi kwa ujumla wenye taarifa zozote zinazoweza kusaidia uchunguzi, kuzitoa ili zifanyiwe kazi.




## Mlinzi aliyedaiwa kuuawa na bosi aokotwa msituni akiwa amekufa

**Na Julieth Mkreri, KIBAHA**

MWILI wa mlinzi wa kampuni ya ulinzi ya Homasa, Salim Haji (29), anayedaiwa kupigwa risasi na bosi wake umeelezwa kuwa umeokotwa Misugusugu, Kibaha mkoani Pwani.

Tukio la Haji kupigwa risasi na bosi wake anayejulikana kwa jina la Andron Mendes, linadaiwa kutokea Novemba 20 akiwa lindoni eneo la kuhifadhia mitungi ya gesi, Tegeta Scanska, Kinondoni, Dar es Salaam, alikokuwa anafanyia kazi ya ulinzi.

Akizungumza na Nipashe jana mjini hapa, baba mdogo wa marehemu, Ramadhani Shehoza, alisema tangu kutokea kwa tukio hilo, wamekuwa wakimtafuta ndugu yao bila mafanikio na mara kwa mara wamekuwa wakifika kwenye vituo vya polisi Madale, Mabwepande na Oysterbay.

Kwa mujibu wa Shehoza, Desemba Mosi alipigiwa simu na ndugu yake aliyemtaja kwa jina la Ibrahim Ally, akimweleza kuwa kuna mtu aliona gazeti la Nipashe kuhusiana na mlinzi kupigwa risasi na mwili wake haujapatikana na taarifa za miili iliyookotwa huko Kibaha.

Alisema mtoa taarifa huyo aliwataka ndugu kufika Kibaha kufuatilia uwapo wa taarifa za miili iliyookotwa kipindi cha mwezi Novemba.

Baada ya kupata taarifa hizo, alisema aliwatuma ndugu wawili kwenda kulizia kituo cha polisi Kibaha ili kupata taarifa kamili ambao walianzia Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani, Tumbi.

"Walianzia hospitali ya Tumbi walipothibitisha kuwa ndugu yao yupo, walikwenda polisi kutoa taarifa na leo (jana) Desemba 3, tumekuja hapa kuhakikisha. Tumemwona ndugu yetu yupo na ni yeye" alisema.

Shehoza alisema walipofika katika chumba cha kuhifadhi maiti, walibaini mwili wa kijana huyo ukiwa una majeraha ya risasi maeneo ya juu ya sikio iliyopigwa upande mmoja na kutokea upande wa pili.

"Baada ya kujiridhisha, sasa tunasubiri taratibu za kipolisi wao ndio wataturuhusu kuchukua mwili kwenda kuuzika kijijini Ngwelo B, Kata ya Tamota, Halmashauri ya Bumbuli (mkoani Tanga)," alisema.

Alisema Haji ameacha mke na watoto wawili ambao kwa sasa wako Kijijini Ngwelo B.

Baba mdogo huyo alibainisha kuwa Haji alikuwa tegemeo kwa familia yake akiwamo mama yake mzazi ambaye anaumwa kwa muda mrefu na kwamba alikuwa anamtegemea kulea familia.

Faraji Utanda, kaka wa marehemu, alisema baada ya kupewa taarifa na baba yake mdogo, Ramadhani Shehoza, juzi alifika hospitali ya Tumbi ambako walielekezwa kufika chumba cha kuhifadhia maiti kutambua mwili wa ndugu yao.

Nipashe ilipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, kwa njia ya simu alisema bado hajapata taarifa za kuokotwa kwa mwili huo.`

# Wasiojulikana waiba mtoto mchanga

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

MTOTO Benitha Benedict, mwenye umri wa mwezi mmoja ambaye ni mtoto wa Joanitha Agustina, mkazi wa Mtaa wa Migera, Kata ya Nshambya, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, ameibwa na watu wasiojulikana wakati mama huyo alipokuwa akiwasindikiza wageni.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale, alisema tukio hilo lilitokea Desemba Mosi mwaka huu majira ya saa sita kamili mchana nyumbani kwa mama huyo.

Mwampaghele alisema kwa mujibu wa maelezo ya mama wa mtoto huyo kwa jeshi hilo, akiwa nyumbani anaendelea na shughuli zake, mwanawe alikuwa amelala chumbani wakati huo akipokea wageni watatu wanawake waliofika kwa lengo la kumpongeza kwa kujifungua.

"Akiwa anawasindikiza watatu hao, walikuja tena watu watatu kumtaka mazungumzo akawajibu kwamba hakuwa na mazungumzo nao na akaamua kuendelea na kuwasindikiza wageni wake, wakati anarudi nyumbani akitoka kusindikiza wageni wa awali aliingia ndani mpaka chumbani alipokuwa amelazwa mtoto, hakumwona tena," alisema.

Kamanda Mwampaghale alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa kubaini waliohusika na wizi wa mtoto huyo na kuwataka wananchi kutoa taarifa kuhusu mtu yeyote wanayemtilia shaka.




Katibu wa Chama cha ufugaji kuku kibiashara Tanzania (TCPA), Thabit Batenga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati wadau wa sekta ya uzalishaji wa vifaranga na wafugaji wa kuku, walipokuwa wakijadili changamoto za upatikanaji wa masoko zinazowakabili kutokana na uingizaji holela wa vifaranga kutoka nje ya nchi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Organia Ltd, Albert Momdjian na Meneja Manunuzi wa kampuni hiyo, Oswald Kessy. **PICHA: JOHN BADI**

# Samia ataja kikwazo ukombozi wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali itaendelea kuwashirikisha wanawake kwa kuhakikisha inatanua mtandao wa wanawake katika sekta mbalimbali.

Aliyasema hayo jana wakati wa Kongamano la Nne la Wanawake Vijana wa Mtandao wa Viongozi Wanawake barani Afrika (AWLN) lililofanyika Zanzibar.

Rais alisema lengo la kuwashirikisha wanawake ni kufikia Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu, Ajenda ya Umoja wa Afrika (AU) ya 2063 pamoja na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025.

Alisema maendeleo ya wanawake yamekuwa yakiathiriwa na changamoto mbalimbali kama kutokupata rasilimali, kutengwa, kutokupata haki zao na kutokupewa nafasi katika kufanya uamuzi.

Rais Samia alisema takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2021 idadi ya wanawake walioajiriwa ilishuka, akibainisha kuwa wanawake milioni 45 duniani waliondoka katika ajira mwaka huo na hivyo kuwafanya kuwa maskini zaidi.

Kwa kutambua hilo, Rais Samia alisema Tanzania inafanya jitihada ya kuwashirikisha wanawake katika vyombo vya kufanya uamuzi, akitolea mfano kuongezeka kwa idadi ya wabunge kutoka asilimia 21.5 mwaka 2005 hadi asilimia 37 mwaka huu na mawaziri tisa katika Baraza la Mawaziri.

Alisema jamii bado inawaona wanawake kama mama wa nyumbani na kutaka mitazamo hasi ya namna hiyo inayomkandamiza mwanamke, iondolewe.

"Wanawake wanapitia changamoto nyingi, wengi wakionekana kuwa majukumu yao makubwa ni kuhudumia familia pekee," alisema.

Rais Samia pia alisema wanawake hawashirikishwi kwenye shughuli za ubunifu na uzalishaji mali katika sekta mbalimbali huku katika baadhi ya maeneo wakipoteza maisha na wengine wakijitahidi kupambana katika kupata usawa.

Alikiri wanawake kuwa wachache katika baadhi ya sekta, akilitaja eneo la sayansi kuwa ndilo lenye shida zaidi kwa kundi hilo na kutaka jitihada za makusudi zichukuliwe kuongeza ushiriki wao. Alibainisha kuwa ili kufikia usawa wa jinsia, lazima kundi hilo lipate elimu itakayoliwezesha kufikia malengo yao.

"Tutaendelea kutoa nafasi kwa wanawake kwa kuwa waliopata nafasi wanafanya vizuri katika majukumu yao na kuna fursa nyingi ambazo zinaleta ukombozi, hivyo ni vyema kuwezeshwa katika kufikia fursa hizo," alisema.

Rais Samia pia alisisitiza janga la UKIMWI bado ni tatizo nchini, wanawake, hasa wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 wakiwa hatarini zaidi.

Rais wa Shirikisho la Ethiopia, Sahlework Zewde alisema ipo haja kuwashirikisha viongozi vijana ili kuwapata wazuri wa baaadaye katika nyanja mbalimbali za uongozi barani Afrika.

Pia alisema kuna haja kupunguza vikwazo vinavyowakumba wanawake ili kufikia malengo hayo ikiwa ni pamoja na kuwafungulia fursa mbalimbali na kuwashirikisha katika shughuli za uongozi.

Mwakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (EU), Zlatan Milisic alisema Tanzania imepiga hatua katika kuweka usawa wa wanawake na kutaka mataifa mingine kuiiga.

AWLN ni mtandao unaotaka wanawake wawe na sauti katika nyanja zote za maisha kwa kutekeleza Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na kufikia Malengo ya AU ya kufikia Afrika tunayoitaka.

# Watiwa mbaroni tuhuma kuingia Tanzania kinyemela

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limewakamata wahamiaji haramu 12 kutoka nchi nne tofauti wakisafirishwa na madalali wa biashara hiyo kupelekwa Afrika Kusini kwa ajili ya kutafuta kazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi wa Polisi Stellah Mutahibirwa, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema wahamiaji hao walikamatwa juzi Desemba 2 mwaka huu majira ya mbili usiku eneo la Sabasaba katika Manispaa ya Singida.

Alisema wahamiaji hao kutoka Ethiopia, Eritrea, Somalia na Kenya walikamatwa wakati askari wakiwa katika doria za kuimarisha ulinzi wakisafirishwa kutoka mkoani Arusha kupitia Singida, Mbeya na baadaye kuvushwa kupelekwa Afrika Kusini.

Kamanda Mutahibirwa aliwataja wahamiaji hao kutoka Somalia kuwa ni Hodam Adam (17), Mohammed Abdul (17), Mohammed Abi (17), Said Abdallah (15) na Abdulhaman Ally (20) na Bamoo Hafu kutoka Ethiopia.

Wahamiaji wengine kutoka Eritrea ni Joel Daniel (24), Emmanuel Kidai (25), Aron Yonas (23) na kutoka Kenya ni Tamiru Garimaa (19), Ally Adam (19) na Yusuph Said (17).

Alisema baada ya kuwakamata na kuwahoji, walisema walikuwa wakipelekwa Afrika Kusini kwa ajili ya kutafuta kazi.

Kamanda Mutahibirwa alisema Jeshi la Polisi linaendelea kuwahoji zaidi wahamiaji hao pamoja na madalali ili kubaini sababu za kujihusisha na biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu na kujua mmiliki wa gari lililotumika kuwasafirisha ili hatua za kisheria zichukukiwe dhidi yao.

Aliwaomba wananchi mkoani Singida kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwafichua wahalifu ili hatua za kisheria ziwe zinachukuliwa na kuufanya mkoa kuwa na amani.

# Unyanyasaji wafanyakazi washtua

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ametoa maagizo saba kwa waajiri ikiwamo kutenda haki kwa waajiriwa kwa mujibu wa sheria na kuacha kuwanyanyasa.

Ametolea mfano matukio mawili yaliyofika mezani kwake ya mwajiri kudaiwa kulazimisha ngono kwa mwajiriwa.

Aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa sherehe za utoaji wa Tuzo za Mwajiri Bora wa Mwaka 2022 zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE). Kampuni ya Vinywaji Baridi ya Coca-Cola iliibuka mshindi katika kipengele cha Ubora Katika Usimamizi wa Rasilimali Watu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mpango aliwataka waajiri kuacha vitendo vya uonevu, unyanyasaji na ukatili pahala pa kazi, akibainisha kuwa vitendo hivyo bado vipo ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka ambavyo husababisha wafanyakazi kuwa wanyonge.

"Tumeshuhudia waajiriwa kunyanyaswa kwa ajili ya umri, jinsia, rangi, kabila na hata ulemavu, hakikisheni vinakomeshwa, lazima muweke mifumo itakayowezesha mfanyakazi kutoa taarifa anaponyanyaswa au kuonewa.

"Wiki mbili zilizopita nilipokea barua kutoka taasisi mbili tofauti ambazo wafanyakazi wanalalamika mkubwa wao anawanyanyasa sana, anatafuta ngono kwa lazima, upendeleo, haya mambo bado yapo, msiyafumbie macho kazini," aliagiza.

Makamu wa Rais pia aliwataka watoe haki zinazostahili kwa wafanyakazi kwa mujibu wa mikataba ya kazi kwa sababu ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi mbalimbali walioachishwa kazi, kuchelewa au kudhulumiwa haki zao.

"Tukumbuke kuwa haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa, tunapoadhimisha sherehe hizi za waajiri bora, niwakumbushe waajiri wote kutenda haki na kwa kuzingatia sheria zetu za kazi," aliagiza.

Aliwataka waajiri kuzingatia sheria zilizopo kuhusu ajira kwa wageni kwa kuwa baadhi yao wamekuwa wakiajiri wageni hata katika nafasi zisizo za kitaalamu au utaalamu wake unaweza kupatikana Tanzania.

Alimtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako pamoja na timu yake wawe wanafuatilia taarifa hizo na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alitaka kazi zinazohitaji wataalamu kutoka nje, waajiri waandae mpango wa wataalamu wa taaluma zao watakaochukua nafasi hizo baada ya mikataba kuisha kama sheria inavyoelekeza.

"Jambo la nne, muendelee kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na tija yao ya uzalishaji, serikali imeondoa baadhi ya tozo ili kuboresha mazingira ya uzalishaji na kuongeza tija, waajiri muangalie namna ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi," aliagiza.

Jambo la tano ni kuhusu mikataba, akiwakumbusha waajiri kuzingatia sheria na kuitoa kwa kazi zinazostahili hilo badala ya kuwafanyisha kazi watu kama vibarua.

Pia aliiagiza wizara yenye dhamana ya kazi kutoa elimu kwa waajiriwa kujua haki zao na kuhakiki aina ya mikataba inayotolewa ili ikidhi vigezo vyote muhimu ikiwa ni pamoja na kuainisha wajibu wa mwajiri na haki ya mwajiriwa kwenye masuala ya afya, likizo, ulemavu, mafao na migogoro.

Dk. Mpango pia alisisitiza wafanyakazi kujengewa uwezo na kuhakikisha wanapewa vitendea kazi vinavyohitajika ili wafanye kazi kwa usalama.

Alisema serikali inategemea kuona nguvu kazi yenye uzalendo, utendaji bora, uadilifu na ufanisi wa fani mbalimbali, akiwataka wajiepushe na vitendo vya rushwa, ufisadi na kuhujumu uchumi wa nchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran alisema lengo la utoaji wa tuzo hizo ni kuwatambua wanachama waliofanya vizuri katika kuweka mikakati bora yenye kuthamini usimamizi wa rasilimali watu na shughuli za kibiashara.

Waziri Ndalichako alisema serikali imeshakamilisha upangaji wa kima cha chini cha mshahara kwenye sekta binafsi na kutangazwa katika gazeti la serikali na utekelezaji wake utaanza mwezi Januari mwakani.

"Kazi hii ilikua shirikishi, ATE mlishiriki kikamilifu na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), niwasihi kwamba itakapofika Januari Mosi 2023 sote tutekeleze amri ya kima cha chini cha mshahara sekta binafsi, wasije kujitokeza waajiri ambao hawako tayari kutekeleza wakati kazi hii imefanyika kwa pamoja.

"Mara ya mwisho amri ya kupandisha kima cha chini cha mshahara ilitolewa mwaka 2013, tunaitoa kwa kutambua hakijawahi kutolewa kwa miaka tisa iliyopita.

"Sitegemei nishushiwe barua ya mwajiri anasuasua katika kutekeleza, kwa sababu zipo nyingi, inafika sehemu mpaka viongozi tunawasumbua kwa mambo tulipaswa kuyatekeleza wenyewe," aliagiza.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipokea tuzo ya shukrani kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kutoka kwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, kwa kutambua mchango wa Rais, katika mafanikio ya sekta binafsi nchini, wakati wa maadhimisho ya siku ya Sekta Binafsi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mpango: Wafanyabiashara wanatoa rushwa ili kupewa zabuni za serikali

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amesema baadhi ya wafanyabiashara wanashirikiana na watendaji wa serikali kutoa na kupokea rushwa ili kupata zabuni mbalimbali au kujinufaisha kwa namna moja au nyingine.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam juzi wakati wa Siku ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSD22) iliyoandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) chini ya Mwenyekiti wake, Angelina Ngalula.

Hafla hiyo ilikutanisha wafanyabiashara na wawekezaji mbalimbali na wadau tofauti wa sekta hiyo wa kitaifa na kimataifa, tuzo mbalimbali za kutambua kampuni na vyama vya biashara (PSO) vilivyoonyesha utendaji wa kipekee, zikitolewa.

Katika hafla hiyo, Dk. Mpango alizungumza mambo manane yakiwa ni maelekezo kwa sekta binafsi na wizara mbalimbali ili kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kuimarika zaidi.

Miongoni mwa mambo aliyoyataja ni suala la rushwa, akiitaka sekta binafsi ishirikiane katika mapambano dhidi ya kadhia hiyo.

"Ni kweli baadhi ya wafanyabiashara wanashirikiana na watendaji wa serikali kutoa na kupokea rushwa ili kupata zabuni mbalimbali au kujinufaisha kwa namna moja au nyingine.

"Kulingana na biashara zenu na shughuli zenu za kila siku, ninajua mnaifahamu mianya mingi ya rushwa. Kwa hiyo, ninawakumbusha hao wachache tuache kutoa au kupokea rushwa na wengine wote tutoe ushirikiano kwa TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), kufichua na kukomesha vitendo hivyo.

Aliwataka wahamasishane na kuzipatia uzoefu kampuni zinazochipukia ili kuongeza wigo wa sekta binafsi kwa kuwa wanaamini kukua na kukomaa kwa taasisi hizo changa ni chachu ya mageuzi makubwa baadaye.

Dk. Mpango pia alitaka kuwe na kasi ya utekelezaji mpango wa maboresho katika biashara (Blue Print), akiiagiza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambayo ndiyo wenye dhamana ya kusimamia hilo, ihakikishe inatekeleza shughuli zilizopangwa angalau zifikie asilimia 50 mwezi Desemba mwakani kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 13.

Alisema serikali inadhamiria kufanya kazi na sekta binafsi katika miradi mbalimbali ya ubia ikiwamo ujenzi wa barabara na miradi ya nishati.

"Ikibidi si vibaya twende kujifunze nje kwenye nchi nyingine ambazo zimepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa miradi ya ubia, mfano Ivory Coast ni mojawapo katika bara hili miradi ya ubia imeshika kasi kubwa," alisema.

Makamu wa Rais alisema sekta binafsi haifanyi vizuri katika kuchangamkia fursa mbalimbali na rasilimali za kimataifa katika kulinda mazingira na kuwahamaisha kuzichangamkia rasilimali fedha za kulinda mazingira.

Pia alisema baadhi ya wafanyabiashara wanakwepa kodi na kuwataka kuzilipa kwa hiari na kwa wakati kwa kuwa vitendo vya ukwepaji kodi ni uvunjifu wa sheria.

"Serikali inatimiza wajibu wake wa kuondoa kodi na tozo zisizo na tija na kufanya mfumo wa kodi uwe rafiki kwa wawekezaji na wafanyabiashara, tunawasisitiza nanyi mtimize wajibu wenu wa kulipa kodi kwa wakati," alisema.

Dk. Mpango alisema kuna mfumo ambao umeidhinishwa na serikali wa kuwezesha midahalo baina ya sekta hiyo na serikali chini ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) lakini umekuwa hautumiki ipasavyo, badala yake baadhi yao wamekuwa wakitafuta ufumbuzi wa kero kwa njia zisizo rasmi.

Aliwataka TNBC na TPSF wabaini kwa nini mfumo hautumiki kama unavyotakiwa kwa kuwa ukitumika vizuri utatatua kero na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Dk. Mpango alisema wakati nchi inafunguka kimataifa, hawana budi kujiimarisha ili kuwa washindani katika masoko.

Alisema serikali inaendelea kulipa madai ya zabuni ya fidia za kodi kwa wanaostahili ili kutoathiri shughuli za uzalishaji na utoaji huduma.

Waziri Kijaji alisema biashara siyo vita na kuwataka wafanyabiashara wakubwa kuwashika mkono wale wadogo ili nao wakue na kujenga uchumi wa nchi.

## HABARI KITAIFA




Meneja wa Biashara Tigo Pesa, Restuta Kedmond (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya shilingi milioni moja kwa Jeni Mgonja, aliyeibuka mmoja kati ya washindi nane wa wiki wa promosheni ya "Ndinga la Kishua" inayoendeshwa na Tigo kwa kushirikiana na kampuni ya Hisense, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyabiashara aliyetishia kuua atiwa hatiani kortini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Ilala imemtia hatiani Mfanyabiashara wa Kariakoo, Adelard Lyakurwa kwa kosa la kutishia kumuua kwa bastola mfanyabiashara mwenzake, Valence Lekule.

Hukumu hiyo ilisomwa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Fadhili Luvinga kwa niaba ya Hakimu Mkazi, Glory Mkwera ambaye yuko kwenye kazi maalum.

Hakimu Luvinga alisema mshtakiwa anakabiliwa na shtaka moja la kutishia kuua kwa bastola, ikidaiwa kuwa Julai 30, 2020. maeneo ya Kariakoo, kwa nia ya kutaka kuua alimtishia kwa bastola Valence Lekule.

Alisema katika kesi hiyo upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi wanne na upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi watatu.

"Baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili, mahakama imeona upande wa Jamhuri umethibitisha mashtaka bila kuacha shaka, hakuna shaka kwamba kulikuwa na tishio la kutumia bastola.

"Mahakama imeona mashahidi wa Jamhuri wa kuaminika na ushahidi wa upande wa utetezi hauna mashiko.

"Mahakama imeridhika kwamba upande wa Jamhuri umethibitisha kosa dhidi ya mshtakiwa, hivyo mahakama inamtia hatiani," alisema Hakimu Luvinga.

Akiomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake, Wakili Richard Mbuli alisema ni mkosaji wa mara ya kwanza, anasumbuliwa na maradhi ya vidonda vya tumbo na presha na familia inamtegema, hivyo aliomba apewe adhabu ndogo.

Akitoa adhabu, Hakimu Luvinga alisema mahakama imezingatia hoja zilizowasilishwa, inampa adhabu ya kifungo cha miezi 12 jela au faini ya Sh. milioni moja.

Pia alisema mahakama inaamuru kielelezo cha silaha na kitabu chake vitaifishwe, vitakabidhiwa kwa mamlaka inayohusika. Mshtakiwa alifanikiwa kulipa faini na akaachiwa huru.

Hata hivyo, akizungumza baada ya hukumu hiyo, Lekule alidai hakuridhishwa na uamuzi wa mahakama na anatarajia kukata rufani.

# Wafa wakikamata kumbikumbi

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

WATU wawili, akiwamo mjamzito, wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa katika Kata ya Mahembe wilayani Kigoma baada ya kugongwa na pikipiki wakati wanakamata kumbikumbi pembezoni mwa barabara iendayo Gereza la Kwitanga karibu na Mto Kaseke.

Tukio hilo limetokea karibu na eneo la kichuguu ambacho wakazi wa eneo hilo hukamata kumbikumbi kila msimu wa masika unapoanza.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Kigoma, Filemon Makungu alisema vifo hivyo vya Neema Moshi (18) na Sia Ramadhan (20) vilisababishwa na dereva anayejulikana kwa jina la Yeovan Kagizo (28), akiwa anaendesha pikipiki yenye namba za usajili MC 602 CPJ kwa mwendo mkali, alishindwa kuimudu na kusababisha ajali iliyosababisha vifo.

"Tukio hilo liliripotiwa Novemba 30, 2022 majira ya saa sita mchana ambapo dereva huyo alishindwa kupishana na bodaboda mwenzake katika barabara ya Mahembe - Kwitanga kwa sababu alikuwa katika mwendo kasi na kuwagonga wanawake wawili miongoni mwa wengi waliokuwa pembezoni mwa barabara wakifanya shughuli zao za kuokota kumbikumbi na kusababisha ajali na kisha kufariki dunia walipokuwa wakipata matibabu katika Kituo cha Afya cha Bitale," alisema.

Kamanda Makungu alisema Jeshi la Polisi linamshikilia dereva huyo kwa hatua zaidi na kutoa rai kwa madereva bodaboda kuendesha kwa kufuata taratibu na kanuni za usalama barabarani na kuzingatia mwendo unaokubalika kwenye makazi ili wadhibiti pikipiki zao na kuepusha ajali.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mgawa, Kijiji cha Mahembe Kati, Simon Daniel alisema wamesikitishwa na tukio hilo ambalo ni la pili kutokea eneo hilo kwa ajali zitokanazo na vyombo vya moto, likitanguliwa na la mwaka 2020 ambalo mwanamke mmoja aliyekuwa akienda sokoni kuuza nyanya, aligongwa na gari na kupoteza maisha.

"Sasa ajali imewachukua wengine wawili huku mmoja wao (Neema Moshi) akiwa na ujauzito wa takribani miezi mitano, inatuumiza sana, ninawaomba wananchi tuwe makini tunapotembea barabarani kuepusha ajali," alisema. Shuhuda wa tukio hilo ambaye pia alipata majeraha kwenye mguu kutokana na ajali hiyo, Salma Stephano alisema: "Kama ilivyo kawaida kwa kichuguu hicho kutoa kumbikumbi kila mwaka, siku hiyo pia kilitoa kumbikumbi ambapo wengi wao walikusanyika katika eneo hilo la Kaseke pembezoni mwa barabara kilipo kichuguu na kukizunguka huku tukiendelea kuwakamata kwa lengo la kuwala na biashara, ghafla tulipoo pikipiki ikitufuata kwa kasi na kisha nikapoteza fahamu.

"Nilipopata fahamu kulikuwa na mtu mmoja amechomwa na chuma kwenye mguu kama mimi, mwingine amelaliwa na pikipiki, baadaye nikaona wengine wawili wamelala chini wakiwa wanapepewa, nilisaidiana nao, baada ya muda walichukuliwa na bodaboda na kupelekwa Kituo cha Afya Bitale, haikupita muda mrefu tukaambiwa wamefariki (dunia)."

**KUPOTEA KWA CHETI CHA TAASISI YA UKUMBUSHO WA ZAKA TANZANIA**

**KOMBO HUSSEIN NKUMILWA**

Anatangaza kupotelewa kwa Cheti cha taasisi ya ukumbusho wa zaka Tanzania chenye namba za usajili SA19411 kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa polisi au piga simu namba **0717337919.**

**MOR/MOR/RB/466281/2022.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MAGRETH BAHATI MUNISHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CROWN** yenye usajili namba **T373 EAX**, CHASSIS NAMBA: **GRS2000008344** na ENGINE NAMBA: **4GR0476960.** Kwa yeyote atakaeiona atope taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/453286/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. MMC/LD/33823**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA:MPENA ANDREW WA S.L.P 166, MOROGORO**
**ARDHI: KIWANJA NA. 41 KITALU E KINGOLWIRA MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: ROSE GABRIEL LYIMO WA S.L.P 166, MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa SIKU 30 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO ikionekana, irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA-MOROGORO S.L.P166 MOROGORO

Valency H.K
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

**LEGENDS AUCTION MART AND GENERAL BROKER LIMITED**

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara wa kuuza dhamana zao za magari yaliyopo Vingunguti Dar es salaam na Sinai Mabatini Mwanza SIKU ZA TAREHE 19/12/2022 na TAR 23/12/2022 kuanzia saa tano kamili asubuhi na kuendelea

| S/N | JINA LA MTEJA | MODEL | USAJILI | MAHALI LILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | STANSLAUS DANIEL LUSUMO | LP 909/49 | T335DYA | DAR ES SALAAM |
| 2. | AHMED ABDULRAHMAN HARUNA | LP 909/49 | T779DXE | MWANZA |
| 3. | SAMWEL KISAKA MZAVA | LPK 2519 | T598DMK | MWANZA |
| 4 | JULIUS GAMBA MUGETA | LPT709 | T548DXP | MWANZA |
| 5 | SASN AUTO GARAGE COMPANY LIMITED | NOVUS 340HP | T275DVM | DAR ES SALAAM |
| 6 | ISAYA LWIDIKO SANGA | LP909Bus | T424DNM | DAR ES SALAAM |
| 7 | YAMIN MOHAMED SULEIMAN | UTRA BUS | T728DVN | DAR ES SALAAM |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 na ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa
3. Gharama ya kukagua na kuona magari ni ya mnunuzi pamoja na kuhamisha umiliki ni ya mnunuzi.
4. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote akatayejaribu kuharibu mnada huu
5. Kwa mawasiliano zaidi piga number **0714939933 au 0713857349**

POSTAL HOUSE | 5TH FLOOR, OFFICE NO. 1507 | PLOT NO. 6/7
OHIO STREET / GHANA AVENUE | P.O.BOX 80310 - DAR ES SALAAM
MOBILE: 0714939933 | 0788411524 | 0763243900
Email:legendsab20@gmail.com

117177302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu itolewe madhara ya kuacha kutumia ARV

**DESEMBA** Mosi, mwaka huu, Tanzania iliungana na nchi zingine duniani kuadhimisha Siku ya Ukimwi Duniani, ambayo kitaifa ilifanyika mkoani Lindi huku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi.

Mbali na maadhimisho hayo kufanyika kitaifa mkoani humo, pia mikoa mbalimbali iliandaa na kufanya shughuli hiyo katika maeneo mbalimbali huku ujumbe mkubwa ukiwa kuhamasisha jamii kujikinga na ugonjwa huo ambao tangu ulipotanganzwa miaka ya 1980, umeteketeza nguvu kazi ya taifa wakiwamo wasomi na mataalamu waliokuwa wakitegemewa katika maendeleo ya nchi.

Msisitizo mkubwa katika kujikinga huko ni watu kupima na kutambua hali ya afya zao, kuanza kutumia dawa za kufubaza virusi (ARV), kuchukua tahadhari kwa wale ambao hawana maambukizi na kuacha kuwanyanyapaa wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU).

Pamoja na kuwekwa mkazo katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo, jambo ambalo lilishtua na kuleta taharuki ya kuwapo hatari zaidi ni taarifa kwamba baadhi ya watu waliokuwa wakitumia ARV wameacha kufanya hivyo.

Katika mkoa wa Njombe, mathalan, ilibainishwa kuwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (WAVIU) 291 kati ya 16,594 waliokuwa wakitumia dawa hizo, katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, wametoroka kwenye huduma za dawa kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuaminishwa na viongozi wa dini kuwa wamepona baada ya kufanyiwa maombi. Watu hao ni wanaume 104 na wanawake 187.

Kutokana na watu hao kukimbia, idara ya uratibu wa Ukimwi kwa sekta zote katika halmashauri hiyo, ilisema imechukua hatua za kuanza kuwafuatilia ili warejee na kuendelea kutumia dawa hizo.

Taarifa za watu kuacha kutumia ARV zimezua taharuki na zinaonyesha kurudisha nyuma juhudi za kupambana na ugonjwa huo. Takwimu zilizotolewa kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe ni sampuli ndogo ambayo inaakisi kwamba tatizo hilo liko katika maeneo mbalimbali nchini.

Hatua hiyo inaonyesha kuwa kuna uwezekano wa kuibuka kwa vifo vya watu kwa sababu ya kuacha kutumia dawa hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zimewezesha waliokuwa katika hali mbaya kiafya kutokana na kinga ya mwili kupungua, walirejesha matumaini na kuendelea kuishi na kufanya shughuli zao za kila siku.

Kuwapo kwa taarifa hizo kuwashtue viongozi wa serikali na wadau wengine wa mapambano dhidi ya Ukimwi na kuaza kuchukua hatua. Wahenga wanasema mzaha mzaha hutumbua usaha. Kwa mantiki hiyo, kama jambo hilo linaweza kuachwa bila kufanyiwa kazi , kuna hatari tukashuhudia maafa zaidi.

Miongoni mwa hatua zinazopaswa kuchukuliwa ni dhidi ya viongozi wa dini wanaowadanganya wanaotumia dawa kwamba wamepona baada ya kufanyiwa maombi. Watu hao walioibuka kwa majina ya mitume na manabii, wamekuwa na nguvu kushwawishi watu kuwasikiliza lakini katika hilo lazima wachukuliwe hatua.


Sambamba na hilo, ni vyema elimu zaidi itolewe na wataalamu juu ya athari za kuacha kutumia dawa hizo kwa wale walioanzishiwa dozi pamoja na kuwahimiza kuachana na mafundisho yenye upotoshaji kwa sababu yana hatarisha maisha yao.

Kwa ujumla, jambo hili linalosababishwa na mafundisho yenye kupotosha ni hatari kwa ustawi wa taifa kwa sababu kitendo cha kuwaaminisha watu kwamba wamepona, kinaweka mazingira ya watu kuamini hivyo na kuendelea kuwakimbilia viongozi wa dini kwa madai ya kuombewa na matokeo yake, umati wa watu kuacha kutumia dawa.

Ni vyema sasa serikali ikachukua hatua madhubuti katika kudhibiti tatizo hilo ili kuwalinda watu wake dhidi ya mafundisho yasiyofaa.

Kila mtu ana imani yake lakini linapofikia suala la kuaminishwa kupona Ukimwi, ni baya na linapaswa kukemewa kwa nguvu zote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mzaha huu wa kuvuka barabara eneo la Mbezi Mwisho ni hatari

**BARABARA** ya Morogoro imepanuliwa kuanzia Kimara Mwisho Dar es Salaam hadi Kibaha Maili Moja mkoani Pwani, kwa lengo la kupunguza foleni za magari kwenye barabara hiyo.

Upanuzi huo umekwenda sambamba na ujenzi wa madaraja matano kwenye barabara hiyo, yakiwamo mawili ya waenda kwa miguu na matatu ya magari yaliyopo Mbezi Mwisho, Kwa Yusuph na Kimamba CCM.

Madaraja ya waenda kwa miguu, moja lipo Kimara Mwisho na lingine Mbezi Mwisho, ambayo pembeni mwake umejengwa uzio ili kuhakikisha kila mmoja anayatumia, ili kuepuka kugongwa na magari.

Hata hivyo, pamoja na serikali kufanya juhudi hizo zenye lengo la kupunguza foleni za magari na kuepusha waenda kwa miguu dhidi ya ajali za barabarani, bado wapo baadhi ya watu wanaoendelea kuhatarisha maisha yao.

Watu hao ni wale wanaokatisha barabara hiyo eneo la Mbezi Mwisho na kupenya kwenye uzio huo badala ya kupita juu ya daraja, kitendo ambacho ninakiona kama ni hatari kwa usalama wao.

Mbali na hao wanaopenya kwenye uzio, wengine wanalala chini kwenye maeneo ya kupitisha maji ya mvua yanayotiririka kutoka barabarani kwenda mtaroni ambako vyuma vya uzio huo havifiki na kupenya.

Kwa mtindo huu, ninadhani ipo haja kwa watu kubadilika na kuacha mazoea ambayo mwisho wake unaweza kuwa ni hatari, kwani ni ajabu kuona watu wanaendelea kupenya kwenye uzio kuvuka barabara wakati daraja lipo.

Ikumbukwe kuwa uzio huo umeweka pande mbili za barabara hiyo kuanzia njiapanda ya kuelekea Goba hadi Kwa Yusuph, ili kuhakikisha hakuna mtu anayeonekana ndani ya uzio huo.

Lakini cha kushangaza, bado wapo wanaoendelea kuonekana humo na wengine kupenya na kuvuka upande wa pili wa barabara wakati daraja lipo, kitendo ambacho kinaweza kuhatarisha maisha yao.

Ingependeza kama jamii itaacha kuishi kwa mazoea, badala yake izingatie taratibu, kanuni na sheria kuliko kila mtu kufanya jambo anavyojisikia au anavyotaka, huku akijua kwamba anakwenda kinyume.

Mazoea ndio ambayo yamekuwa yakisababisha watu kufanya lolote wanalojisikia, ikiwamo hata kufanya biashara katika maeneo ambayo kuna tangazo linalowataka wasiwepo eneo husika.

Vilevile kwa mazoea hayo, wapo wengine ambao huvuta sigara hata kwenye eneo ambalo lina tangazo kuwa ni marufuku kuvutia sigara au kuvuka eneo lililowekewa utepe kwa maana ya kutoruhusiwa kupita.

Mtindo huo wa kuchezea mazingira hatarishi, ninadhani waliozoea hivyo wanatakiwa kuelimishwa ili kutambua madhara yake kuliko kuendelea kuhatarisha maisha yao bila sababu ya msingi.

Kwa mfano, mtu anaona daraja la waenda kwa miguu lipo, lakini analiacha na kuvuka barabara kwa kulazimisha kupenya kwenye uzio, ambao umewekwa ikiashiria kwamba njia ya kuvuka eneo husika ni kupita juu ya daraja.

Iwapo mamlaka husika haitadhibiti mtindo huo, yawezekana kukawa na hatari ya watu kugongwa na magari hasa pale barabara za mabasi ya mwendokasi zitakapofunguliwa na kuanza kutumika rasmi.

Ni vyema kama wanaofanya mchezo huo watatambua kuwa wako katika hatari, ili watumie daraja, kwani wanachofanya ni sawa na kuharibu miundombinu iliyowekwa, ili kila mmoja avuke kupitia darajani.

Ikumbukwe kuwa, kwa sasa hata magari yanayovuka upande wa pili wa barabara, yanapita juu ya madaraja yaliyopo eneo hilo, kitendo ambacho ni wazi yanayotoka au kuingia katikati ya jiji, 'yanajinafasi'.

Hatua hiyo inaonyesha kuwa hakitakiwi kuvuka kitu chochote ndani ya uzio huo, ingawa baadhi ya waenda kwa miguu wameonekana kuwa wagumu na kuamua kulazimisha kupenya kwenye uzio huo.

Wakati hao wakifanya hivyo, baadhi ya madereva wa bodaboda nao hushusha abiria ndani ya uzio na kuwaacha wakihangaika kutafuta jinsi ya kuvuka barabara hiyo na kujikuta wakilazimika kupenya katika uzio.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Tuwe na mtazamo chanya kuhusu mitumba



Pascal Mayalla

KWA "Maslahi ya Taifa" leo ninawafundisha Watanzania kuwa na mtazamo chanya (positive attitude) kwenye kila jambo la heri, badala ya kulalamika, kukosoa, kuponda kila kitu hata vya kitaalam, ambavyo wananchi wa kawaida hawana ujuzi navyo.

Mada hii ninaitoa kutokana na nchi yetu kupokea mabehewa 'mapya' ya reli yetu ya kisasa (SGR) yaliyotoka kiwandani Korea Kusini. Ninatumia neno 'mapya' ili kujulisha kuwa mabehewa mapya haya yanasemekana tu kuwa mapya, lakini Watanzania bado hawathibitishiwi upya wake, hivyo nikiwa mwandishi wa habari, kwenye fani yetu, unashauriwa unapokuwa na shaka kuhusu jambo fulani, usiliandike kwanza, tafuta kwanza uthibitisho, ndipo uliandike. Kwa mantiki hiyo, kuhusu upya wa mabehewa haya yaliyopokewa, bado sijauthibitisha. Katika kutafuta kwanza uthibitisho wa upya wa mabehewa haya, tayari nimeshakutana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, nikamweleza kuhusu jambo hili na amenikubalia nitamtafuta ili kulizungumzia. Wakati nikiisuburi hiyo miadi ya Kadogosa, naomba kwa siku ya leo, nitimize moja ya majukumu muhimu ya vyombo vya habari. Zaidi ya jukumu kuu la kuhabarisha jamii, vyombo vya habari vina wajibu wa kuelimisha jamii, hivyo leo natoa elimu ya kitu kinachoitwa mtazamo chanya kuhusu jambo lolote.

Mabehewa haya 'mapya', yamepokewa na mtazamo hasi na baadhi ya vyombo vya habari hasa magazeti na mitandao ya jamii. Siku mabehewa hayo yanapokewa pale bandarini, nikamsikia Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akigomba kuhusu watu na mitandao ya kijamii wanaoyaponda kuwa ni ya kizamani. Kwenye hili la mabehewa kuwa na muundo wa kizamani, wala halikumhitaji Waziri kugomba kwa sababu huu ni ukweli bayana bila kificho kuwa mabehewa haya licha ya kuwa ni 'mapya' kutoka kiwandani na yamekuja na nailoni zake kabisa za upya, lakini ni ya mtindo wa kizamani. Kwa vile ni TRC wenyewe ndiyo huko nyuma walituonyesha picha za vichwa na mabehewa ya kisasa ya treni zetu za SGR, kilichopokewa ni kitu tofauti na tulichoonyeshwa mwanzo. Wananchi wana haki ya kushangaa, kujiuliza, hata kuponda na kukosoa. Haki hiyo inaitwa kwa kizungu 'legitimate expectations' yaani matarajio hali ya kisheria uliyoyatarajia, ukaletewa kitu cha tofauti au kinyume cha matarajio halali ya kisheria, una haki ya kulalamika, tena kwa wenzetu, una haki hata ya kushtaki mahakamani na ukashinda kesi.

Hata mtu akimwahidi tu msichana kuwa "nitakuoa", baadaye ukabadili mawazo na hukumwoa huyo aliyemwahidi, anaweza kufungua kesi ya madai mahakamani na kudai fidia ya athari alizopata kutokana na kuvunjwa kwa ahadi hiyo. Kwa hiyo Watanzania wanaolalamikia mabehewa haya, wana haki ya kufanya hivyo na wana haki pia ya kuyaponda.

Hali hii ndiyo imenifanya niendeshe somo la mtazamo chanya kwa kuelimisha kuhusu kuwa na mtazamo chanya kuhusu mwonekano wa kitu, usasa dhidi ya uimara, umadhubuti na utendakazi kati ya vifaa vipya (brand new), vifaa vilivyotumika, vifaa chakavu (mitumba), vifaa vya kisasa dhidi ya vifaa vya kizamani na vile vilivyopitwa na wakati.

Tuanzie kwenye bidhaa mbili kuu za nguo na magari. Bidhaa za nguo zilizotumika kwa jina maarufu la mitumba, huletwa nchini zikiwa kwenye makontena, huku ndani zimefungwa kwenye marobota yanayoitwa mabelo.

Japo zote huitwa mitumba, mitumba hiyo ina madaraja mbalimbali. Kuna mitumba ya daraja A kutoka Ulaya na Marekani, daraja B na C. Watanzania wengi kutokana na kupenda vitu vya bei rahisi, wauza mitumba wengi, hupendelea kununua mitumba ya daraja B na C kwa sababu ni ya bei poa. Nchi za wenzetu, kama Kenya na Uganda, wanapokea mitumba ya daraja A pekee, hivyo kuna wauza mitumba wanafuata mitumba ya daraja A Kenya na Uganda. Kuna wachache Tanzania ambao wanaagiza mitumba ya daraja A na mitumba hiyo inauzwa dukani.

Ndani ya mabelo yote ya nguo za mitumba, kuna baadhi ya nguo ni mpya kabisa hazikuwahi kuvaliwa hata mara moja, hivyo kuna nguo mpya lakini ni za mtumba! Tukija kwenye ubora wa hizi nguo, nyingi za mitumba zina ubora wa hali ya juu kuliko hata baadhi ya nguo mpya kutoka China. Kwa hiyo kuna nguo na vifaa vya mitumba, zinauzwa kwa bei ya juu kuliko mpya na ni bora kuliko vitu vya dukani.

Kama ilivyo kwenye nguo, vivyo hivyo kwenye magari, yako yaliyotumika, yaani yametumika kidogo kama mapya na kuna baadhi ya nchi, kuna magari ya kilometa sifuri lakini yanauzwa kama mtumba kwa sababu yamekaa dukani muda mrefu, wakatoa aina mpya, hivyo yale ya muundo wa zamani yote yanapelekwa mtumbani, hivyo tuanze kuwa na mtazamo chanya kuhusu mitumba, si kila mitumba ni chakavu, mitumba mingine ni mipya kabisa.

Nchi tofauti tofauti zinasifika kwa wingi wa vitu tofauti tofauti na ubora tofauti tofauti. Japan ndiyo nchi inayoongoza kwa utengenezaji wa magari ya bei poa. Baadhi ya magari ya Japan, mabati yake ni kama makaratasi, likipata ajali, linaweza kusagika kama chapati. Magari ya Ujerumani, Ulaya na Marekani ni magumu, imara na madhubuti, hivyo baadhi yake yaliyotumika yanauzwa kwa bei ya juu kuliko gari jipya kutoka Japan. Tukirudi kwenye mabehewa yetu, Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, alitueleza ukweli kuwa tumeagiza vichwa vipya na mabehewa mapya, hivyo lazima uweke oda na inachukua muda kutengenezewa. Kwa mantiki hiyo, kwa kuanzia tutaanzia vichwa na mabehewa yaliyotumika. Vichwa hivi na mabehewa haya ni kutoka nchini Ujerumani.

Kwa hiyo haya mabehewa yetu 'mapya' kama ni mabehewa ya chuma cha Mjerumani, hata kama ni mabehewa yaliyotumika na hatukuambiwa, nawaomba Watanzania wenzangu tuyapokee kwa mtazamo chanya kuwa tumeletewa bidhaa bora. Tupokee kwa moyo mkunjufu, tuyakubali kwa kuwa serikali yetu ina nia njema na Watanzania.

Wiki Ijayo, nitawaletea mahojiano yangu na Mkurugenzi wa TRA, Masanja Kadogosa, ambayo pia yataandamana na kipindi cha TV cha "Kwa Maslahi ya Taifa" kuhusu mabehewa haya 'mapya'. **Wasalaam.**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Nampa Samia Udaktari wa Heshima kwa uthubutu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HISTORIA ya Tanzania ni ndefu ikitoka kuitwa Tanganyika na Zanzibar hadi mwaka 1964 viongozi wetu, Julius Kambarage Nyerere na Abeid Amaan Karume walipoamua iwe na ikawa.

Hivyo Tanzania ikaanza kuongozwa na Mwalimu Nyerere ambaye naweza kusema ni kama alianza kujenga nyumba ya nyasi na miti, ikikandikwa na udongo ili mradi Watanzania waliishi kwao kwa raha mustarehe.

Katika nyumba hiyo, kulikuwa na wadudu na wanyama ambao waliingia katika madirisha na milango ya mianzi iliyotumika kuyatengeneza. Hivyo katika nyumba hiyo, Watanzania chini ya viongozi hao tulipambana kuwatimua.

Hata hivyo, katika nyumba hiyo, maisha hayakuwa rahisi sana kwani mwishoni mwa utawala wa Nyerere, nyumba ilivamiwa na binadamu wasio wema kutoka nyumba jirani.

Aliingia mtu akiitwa Idi Amin na majeshi yake na kutuvuruga akitutia ulemavu, akipora mali zetu na kuua baadhi ya ndugu zetu. Tulihangaika na maisha, baadhi yetu tukawa vichaa wa kufukuza magari yaliyokuwa yanagawa unga.

Baadhi yetu kichaa kikitusababisha kupigana pale tulipokuta mawe yameondolewa kwenye foleni ya unga na sukari, bidhaa zilipotea huku aliyekuwa na dawa ya mswaki akionekana mtu wa aina yake. Tilijifunga mikanda tukakondeana.

Nyerere alipoondoka, akamwachia Alhaj Ali Hassan Mwinyi, ambaye alishuhudia hali hiyo ikiwa ngumu mpaka rangi za viatu ikionekana bidhaa adimu, achilia mbali sabuni za kuogea na kufulia. Akatafakari na kuona haiwezekani akatangaza 'hashtag' RUKSA!

Kila aliyekuwa anaweza kuingiza kitu nchini, akaambiwa RUKSA! Kwa nguvu moja akaendeleza alichoanzisha Naibu Waziri Mkuu, Dk Salim Ahmed Salim, kwamba sasa tuingize nguo za Kafa Ulaya, ambazo baadaye kwa jina la heshima tukaziita mitumba.

Watu wakavaa angalau nguo zilizoonekana ni nguo badala ya makaniki kutokana na hali ya kujifunga mikanda kulikosababishwa na majeshi ya Nduli Amini. RUKSA ilifanikiwa sana na mpaka leo inaendelea na Kafa Ulaya haijafa.

Akapambana na uhujumu uchumi akifuata nyayo za Waziri Mkuu wa zamani Edward Moringe Sokoine, akaja na FAGIO LA CHUMA, hii nayo ikakumba wengi waliokula bila kunawa. Ila angalau aliibadilisha nyumba kwa kuezua nyasi na kuezeka mabati.

Alitufikisha mahali Mzee Ruksa akaiacha nchi mikononi mwa Benjamin William Mkapa ambaye hata hivyo alikuta nchi inadaiwa kutokana na hali aliyoikuta Mwinyi, kwani hapakuwa na namna ila kukopa ili kuendana na maisha. Yeye akapambana na nidhamu ya uwajibikaji. Nchi ikakaa sawa kwa kulipa madeni na kurejesha heshima kimataifa.

Alifanya mengi ikiwa ni pamoja na kuendeleza wazo la nchi kuwa na uwanja mkubwa wa michezo lililoasisiwa na Alhaj Mwinyi, tukawa na uwanja mkuu wa Taifa ambao unajulikana kama uwanja wa Mkapa aka Lupaso. Nyumba akaiwekea lipu ya saruji na madirisha ya mbao.

Akaondoka na kumkabidhi nchi Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye alitaka maisha yawe bora kwa kila Mtanzania. Bila shaka alifanya yake, ikiwa ni pamoja na kujenga Diplomasia ya Kimataifa. Nchi ikaheshimika, ikatembelewa, watu wakatembea kujifunza nje.

Angalau maisha yakawa maisha, wananchi wakapumua baada ya kazi kubwa zilizofanywa na watangulizi wake. Naye akaacha wazo la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ikiwa ni baada ya kuleta mabasi yaendayo haraka mnayoyaona hivi sasa. Huyu nyumba akaiwekea marumaru na madirisha ya vioo.

Akamwachia John Pombe Magufuli, akatandika barabara, akajenga madaraja, akatumbua watu, akakataa na kukataza kusafiri nje, akakataa semina na warsha, akazuia siku kuu na sherehe kwamba ni ufujaji wa fedha. Tukaanza kuweka mipini kwenye meno, chini ya HAPA KAZI TU! Tukajiandaa kulimia meno! Nyumba akaichorachora na mirangi na tope.

Kwa kudra za Mwenyezi Mungu, Magufuli naye akaondoka na kwa kudra hizohizo, akaingia Samia Suluhu Hassan. Niseme nini kwa aliyoyafanya Mama huyu, kwani ni mengi kwa kipindi kifupi sana alichoingia madarakani na ndiyo sababu hata hii heshima aliyopewa juzi ya Udaktari wa Heshima ni ndogo.

Katika kipindi chake, meno yamesalimika. Humo magerezani waliobambikwa kesi wametoka. Amekutana na wanasiasa na kuwaambia maendeleo hayana itikadi, tofauti na kabla yake tukiambiwa maendeleo hayaendi kwa wapinzani.

Hivi nikuulizeni mnaobagaza heshima aliyopewa Chifu Hangaya, hivi enzi zile za kupima mapapai kama ATAKE ASITAKE ingechukua mkondo wake leo mngekuwa na chanjo ya UVIKO-19? Leo fedha za UVIKO-19 zingejenga shule, vituo vya afya, barabara, umeme na miundombinu mingine kweli? Maridhiano je? Vyombo vya habari mngetoboa? Ni mengi nami ningempa Mama heshima hiyo kwa uthubutu. Alamsiki!

# Idadi ya watalii yaongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema idadi ya watalii wanaofika nchini imeongezeka na kufikia 1,175,697 kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu kulinganishwa na watalii 922,692 katika kipindi hicho mwaka jana.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya 20 ya Chuo cha Utalii (NCT) jijini Dar es Salam, akisema ongezeko hilo linatokana na programu ya Tanzania The Royal Tour.

"Ukarimu ndiyo kigezo pekee cha mgeni kukaa nchini kwa muda mrefu, hasa kwenye sekta ya utalii. Hotelini, viwanja vya ndege, wasafirishaji wa wageni hawa, kuwapo watoa huduma wenye weledi ni muhimu sana," alisema.

Naibu Waziri alisema kikwazo kilichopo kwenye hoteli, baa na maeneo mengine ya kuwapokea wageni, ni uhaba wa huduma zinazokidhi zilizo na ubora hasa kwa wageni.

"Mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka dola milioni 714.59 (Sh. trilioni 1.644) mwaka 2020 hadi kufikia dola milioni 1,254.4 (Sh. trilioni 2.886) mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 76," alibainisha.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCT, Dk. Florian Mtey alisema mafanikio ya chuo hicho yanajumuisha ongezeko la wahitimu kutoka 176 mwaka 2014/15 hadi kufikia 475 kwa mwaka wa masomo 2021/22.

Alisema idadi ya wahitimu hao itaondoa uhaba wa watoa huduma kwenye sekta hiyo, ikiwamo eneo la ukarimu, mapokezi, utunzaji wa vyumba, mapishi na uokaji.

"Wahitimu mwendane na mabadiliko ya dunia katika kufikia maendeleo, ikiwamo kuzifuata ajira na si kuzisubiri ajira ziwafuate mlipo, tafuteni fursa, bado kuna maeneo mengi ya sekta hii yana ajira," alisema Mtey.

Kwa mujibu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Sekta ya Utalii inachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa huku ikiingiza asilimia 25 ya fedha zote za kigeni nchini.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhi tuzo ya utoaji huduma za jamii kwa sekta binafsi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire, katika maadhimisho ya Siku ya Sekta Binafsi, iliyoandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), jijini Dar es Salaam juzi jioni. Wengine ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa Fedha wa Vodacom, Hilda Bujiku (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri akerwa kasi ndogo polisi migogoro wakulima na wafugaji

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni amelitaka Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma kuwakamata wafugaji wanaoingiza mifugo katika mashamba ya wakulima na kuwachukulia hatua za kisheria.

Amesema haridhishwa na kasi ya jeshi hilo katika kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji mkoani hapa kutokana na kuwapo matukio mengi ya wafugaji kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima yanayosababisha uharibifu wa mazao, akisisitiza askari hawajatimiza wajibu wao ipasavyo.

Masauni alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali wa wizara yake wilayani Tunduru mkoani Ruvuma alipozuru kutatua mgogoro wa wakulima na wafugaji.

"Kazi yenu polisi ni kulinda raia na mali zao, lakini bado hamnifurahishi katika kushughulika na migogoro ya wakulima na wafugaji. Wananchi wametumia muda mrefu kuandaa mazao yao kwa ajili ya chakula na biashara, wakiuza mazao hayo, nchi itafaidika kwa kodi, lakini wanatokea baadhi ya wafugaji wanaingiza mifugo katika mashamba ya wakulima na kufanya uharibifu mkubwa, hii haiwezekani katika serikali ambayo inataka haki," alionya.

Masauni alisema serikali inawajali askari na imewatendea mambo mengi ikiwamo kukamilisha mahitaji yao ya kupandishwa vyeo, kushughulikiwa kwa stahiki za askari, kutoa mafunzo, kutatua kero ya ofisi na kutoa ajira.

"Mheshimiwa Rais ninampongeza kwa kujali askari, amewajali sana na mnalijua hilo, fanyeni kazi, ni wajibu wenu, mambo mengi ameyafanya mama kwa majeshi yote ikiwamo wizara hii, amewapandisha vyeo askari, ameshughulikia stahiki za askari.

"Kupitia bajeti ameongeza kiasi cha fedha kwa ajili ya stahiki za askari polisi pamoja na vitendea kazi kutoka Sh. bilion 900 mpaka Sh. trilion 1.12 na kuwapo kwa mpango wa kununua magari mapya kwa polisi wilaya zote Tanzania," alisema Masauni.

Waziri huyo pia aliwapongeza askari polisi kwa utendaji kazi wao wanaoufanya na kuwasisitiza kuendelea kufanya kazi kwa weledi kwa kuhakikisha wanawatumikia wananchi kwa kuwa kodi zao ndio zinazofanya kulipwa mishahara na posho mbalimbali.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Alfred Hussein alimshukuru Waziri Masauni kwa kufika mkoani humo na kuahidi kuyatendea kazi maelekezo yote aliyoyatoa katika ziara yake hiyo.

# CRB yakunwa utendaji makandarasi wanawake

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB) imesema inafurahishwa na kasi ya wanawake wanaojitokeza katika kazi za ukandarasi huku ikiwataka makandarasi wa ndani kuwa makini kwenye usimamizi wa fedha.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Consolata Ngimbwa aliyasema hayo juzi wakati wa kufunga mafunzo ya siku tatu kuhusu usimamizi wa fedha kwa makandarasi wa ndani yaliyoandaliwa na bodi hiyo jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa hata mafunzo hayo yaliyohudhuriwa na washiriki 163, idadi kubwa ni wanawake, hali aliyoielezea kuwa inatia matumaini kwamba wanawake wameanza kuona fursa kwenye eneo hilo.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa bila usimamizi mzuri wa fedha, uwezekano wa kutekeleza miradi kikamilifu unakuwa mdogo na hata ukikamilika unakosa unafisi.

"Nimeambiwa kwamba katika mafunzo ya usimamizi wa fedha mlijikita katika uelewa wa taarifa za fedha namna ya kufanya uamuzi wa fedha kwa kuzingatia hali halisi ya taarifa za fedha na usimamizi wa mitaji, haya ni mambo muhimu sana kwa mkandarasi yeyote.

"Mmejifunza pia masuala ya kodi hasa namna nzuri ya kutunza kumbukumbu ili kuepuka kodi zisizostahili au faini kama adhabu kwa kukiuka misingi muhimu ya uandaaji wa hesabu za fedha za kampuni," alisema.

Alisema ujuzi wa kutumia mifumo ya kielektroniki kama mfumo wa ununuzi wa TANePS ni muhimu na mkandarasi ambaye atashindwa kujifunza mfumo huo hawezi kufika mbali kwa kuwa mwajiri mkubwa ni serikali ambaye hutoa zabuni zote kwa njia ya kielektroniki.

Mwenyekiti huyo aliwataka makandarasi kuacha ubinafsi na kuchangamkia miradi mikubwa ya ubia, jambo ambalo litawapa fursa ya kukua kitaalamu na kiuchumi.

"Kutimiza masharti ya zabuni kubwa ni vigumu kwa wengi wetu tunaposhiriki tukiwa mmoja mmoja lakini kwa mfumo wa ubia, tunaweza kuyatimiza masharti hayo na kushindana vizuri," alisema.

Pia aliwataka makandarasi kushikamana na kuunganisha nguvu ili kuwa na sauti moja ambayo itakuwa na uwezo wa kukabiliana na kero mbalimbali zinazowakabili.

Aliwakumbusha makandarasi kujiepusha na vitendo vya kutoa na kupokea rushwa na kuwataka watoe taarifa kwenye vyombo vya usalama pale wanapoombwa rushwa na watoa zabuni.

"Tukifanya kazi kwa kuzingatia weledi na maadili suala la rushwa halitakuwa na nafasi miongoni mwetu, tukikubali kubadilika sote tutaibadilisha sekta yetu ya ukandarasi," alisema.

Naibu Msajili, Utafiti na Maendeleo, David Jere alisema makandarasi waliopata mafunzo hayo, wametoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mtwara, Arusha, Pwani, Lindi, Dodoma, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Songwe, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Manyara, Mara, Mbeya, Tanga na Zanzibar.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea misingi itakayowasaidia kusimamia rasilimali fedha vizuri na kutunza kumbukumbu vizuri ili kuepuka kodi zisizostahili au faini kwa kushindwa kuandaa vyema hesabu za kampuni.

# MAISHA

DESEMBA 4, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

## Furahia tambi za mayai



## Panga ratiba ya usafi wa nyumba uiimarishe

**MAISHA NI NYUMBA** Ukurasa 15




## KATUNIKA


Ukurasa 16



# TUNZA NYWELE NA DAWA

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | L | A | A | N | A |
| | A | | | Y | |
| M | W | A | | U | |
| | A | | I | N | A |
| | M | | | G | |
| S | A | U | M | U | |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, MKE, TAMKA, TENGA, TAKASA, GANDIA


## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI



| | |
|---|---|
| DAFTARI | |
| FUNGUO | |
| BARUA | |
| GOLI | |




# WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO JOHN alikuwa akimsaidia mama yake kupakia asali ndani ya chupa kwa ajili ya kwenda kuuza.

Wakati wanaendelea na kazi ya kupakia asali, John alimuuliza mama yake.

John: Mama hivi asali inatokana na nyuki kwenda kwenye maua?

Mama: Ndio mwanangu, nyuki anapotua kwenye maua anatengeneza asali tamu.

John: Kwa hiyo maua ndiyo yenye asali?

Mama: Hapana ila nyuki hutengeneza asali kutokana na uchavushaji wa maua na kuchukua virutubisho.

Alichokifanya Adaktari

SWALI
Mbuzi dume huwa na alama gani kichwani?



## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia

# Nguvu ya kuchagua ilivyoweka wengi mtegoni

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuangaza duru za Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tuiangalie nguvu ya kuchagua inavyofanya kazi katika maisha yetu ya kila siku.

Kuchagua ni msukumo na ni nguvu iliyo ndani ya mtu. Mungu amempa kila mtu nguvu ya kuchagua. Na nguvu hii imejigawa mara mbili; kuchagua zuri na kuchagua baya. Hapo unapaswa kutafakari unaegemea kwenye upande upi katika kuchagua kwako.

Yupo mtu kwa kutojua nguvu katika kuchagua kitu au kutenda jambo fulani, hujikuta anamwambia mwenzake, "nichagulie wewe au nifanyie wewe". Lakini anapochaguliwa kikawa kibaya analaumu, eti oh! Si alinichagulia fulani? Ebo! Chagua mwenyewe kwani nguvu hiyo imo ndani yako.

Mungu muumba mbingu na nchi amewapa wanadamu zawadi nyingi sana. Mojawapo ni nguvu ya kuchagua. Katika utendaji wetu wa kila siku, yapo mambo ambayo ni lazima tuyatolee uamuzi, iwe ni nyumbani au ofisini.

Pamoja na uhuru wa kuitumia nguvu hii, Mungu mwenyewe ametoa tahadhari katika kuamua kile ambacho unaona kinafaa katika maisha yako. Waweza kuamua jema au kuamua baya na yote hayo Mungu ameyaweka mbele yako uamue mwenyewe unataka kuegemea lipi.

Hebu tafakari Mungu asemavyo katika andiko hili: "Nazishuhudia mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimeweka mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi, chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako" (Kumb.30:19).

Nimeona vijana wengi wanakurupuka hasa katika eneo la uhusiano. Wanashindwa kuelewa kwamba pale kijana anapofikia hatua ya kutafuta mwenzake ili kuoa au kuolewa, yampasa kuwa makini sana katika kuchagua. Ukikosea tu kuchagua pale mwanzoni, majuto yako mwishoni.

Hata wahenga walisema kupanga ni kuchagua; maji yakimwagika hayazoleki; majuto ni mjukuu na haraka haraka haina baraka.

Mungu anatusaidia tuchague nini. Ndiyo maana akasisitiza katika neno lake "chagua uzima, ili uwe hai". Ni ukweli mtupu kwamba wapo watu wanachagua marafiki wasio sahihi na mwishowe wanawaangamiza kisaikolojia, kiuchumi na kadhalika.

Yupo rafiki anayetafuta ukaribu nawe na ukimuamini, lakini kumbe amelenga kuua hatma yako. Atakujia akiomba msaada fulani kumbe ana lengo ovu kuharibu maisha yako! Anakuambia muoe au olewa na yule utaishi maisha mazuri, kumbe anamfahamu ni mbabaishaji!

Nieleweke hapa, sikatazi mtu kuwa na marafiki, lakini nguvu ya kuchagua iliyo ndani yako lazima uitumie vema. Si wote uwaweke karibu kwa maana ya kuwaeleza siri zako. Yafaa kujitafakari mwenyewe ukimwomba Mungu aifanye nguvu ya kuchagua iliyo ndani yako ifanye kazi, ikusaidie.

Hata hivyo, wako watu ambao Mungu hukusaidia ili uwe mbali nao. Lakini pia wapo ambao uliwachagua kwa kuwaamini, japokuwa si sahihi. Unampa taarifa rafiki yako, lakini baada ya muda anakupokonya rafiki, mke au mume wako. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Watu wa aina hii nimeona wakigundua walichagua uamuzi mbaya, pengine wa kujilengesha kwa mume au mke wa mtu, huamua kujiua. Hakuwa na mpango wa kujiua lakini analazimika kuamua kile asichopenda. Hili nitalichambua zaidi wiki ijayo.

Msomaji wangu, wengi wameoa au kuolewa kwa kutumia nguvu ya kuchagua vibaya. Wazazi wengi wamewanyima vijana wao haki ya kuitumia nguvu hii wenyewe na kuwachagulia wenza wao. Matokeo yake ndoa zinasambaratika, kisa hakikuwa chaguo la kijana au binti bali chaguo la wazazi.

Ni lazima mtu achague, lakini mtihani unakuja, nimchague yupi. Wengi wanachagua vibaya baadaye wanajuta, eti ningejua nisingekuoa au nisingeolewa na huyu. Haya ni majuto kwa kuchagua vibaya.

Na watu wengi wanajuta kwa sababu hawakumshirikisha Mungu katika mipango yao ya kimaisha. Wanadhani kwa nguvu na utashi wao wanaweza kufanya kila kitu kikawa sawa.

Moja ya andiko la Mungu linasema: "Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe (Mithali 3:5). Lazima tumshirikishe Mungu kwa yote tufanyayo ili tuwe salama kwani peke yetu hatuwezi.

Mshirikishe Mungu unapotaka kuamua kitu ili usipoteze mwelekeo wa maisha yako. Hakuna jambo linalomshinda kwani kwake yote yanawezekana.

Msomaji wangu, bila shaka umepata mwanga kuhusu nguvu ya kuchagua ndani yako. Wiki ijayo nitaendeleza mada hii. Usikose. Je una **kisa? Ujumbe 0715268581**



## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari

# Waziri Gwajima aungwe mkono ameimudu wizara yake kwa kukabili ukatili wa kijinsia

MTU anayefanya jambo kwa moyo wote na akili yote, huonekana kwa matendo yake, kuongea kwake na lugha ya mwili. Anafanya hivyo kwa kuwa analipenda jambo kwa kulivaa kama lake daima. Katika kufanya hivyo, kila mtu ataona wala hatahitaji kutumia nguvu nyingi kubaini hilo.

Tangu kuundwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimekuwa nafuatilia kwa karibu sana utendaji kazi wa Waziri, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye unapomsikiliza wakati akizungumza, unaona kabisa hili linafanyika kwa moyo wote na akili yote.

Waziri huyu ni mcheshi sana na mara nyingi ana muundo wake wa kuzungumza wenye vionjo ambavyo wakati mwingine humfanya mtu kucheka. Pia anapokuwa kwenye hadhara, anapenda kujichanganya sana na kuchangamsha watu hata kuwaita wafurahi pamoja kama ni jambo lenye kuwafanya watu kujumuika pamoja.

Nimepata nafasi ya kuhudhuria matukio kadhaa ambayo kiongozi huyu ni mgeni rasmi au akijibu maswali bungeni. Wizara yake ni mtambuka inaingia kila eneo na mara nyingi ameonekana mtaani kwa wananchi wa kawaida kabisa waliokumbwa na madhila kwenda kuzungumza na kuwafariji.

Ninaelewa kabisa aliyefanikisha kuundwa kwa wizara hii ni Rais Samia Suluhu Hassan ambaye aliona uhitaji wa lazima ili kuwa na mtu au watu wa kushughulikia masuala ya jinsia kwa haraka, ikiwamo kuweka mikakati madhubuti ya kudhibiti ukatili. Nina ujasiri wa kusema upele umepata mkunaji.

Mara kadhaa, kwa kutaja kwa uchache kulitokea tukio la mwalimu kuwabaka wanafunzi wilaya ya Kinondoni, kwa haraka alifika. Tukio la Shule ya Starlight, Tegeta nako alifika kwa haraka na kutoa maelekezo ya serikali. Pia kuna wanafunzi walikuwa waozeshwe kule Mbagala nako alifika kwa haraka. Mara zote amekuwa mstari wa mbele na anapofika huzungumza na wahusika na si kutuma wasaidizi wake au kusubiri aletewe taarifa ofisini, mara kadhaa ametoa maelekezo ambayo moja kwa moja unaona ni suluhisho la haraka.

Ni waziri pekee ambaye anapokuwa kwenye mikutano au jambo lolote la kikazi, waandishi wa habari wanapotaka kufanya mahojiano naye, hajawahi kuwakatalia au kuwakwepa. Tena wakati mwingine anawasikiliza na kujibu maswali mbalimbali na hata kueleza mikakati na msimamo wa wizara yake ili ueleweke kwa umma.

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya mawaziri na viongozi wengine 'kuwakimbia' waandishi hasa baada ya kuzungumza waliyotaka kuzungumza mbele ya mkutano husika. Wengine hawapokei simu wala kujibu ujumbe wowote unaokwenda kwao na mbaya zaidi hata baadhi ya wasemaji wa wizara na taasisi hizo, ushirikiano wao ni hafifu sana kiasi kwamba umma unakosa haki ya kupata taarifa.

Leo hii mwanahabari akitaka ufafanuzi wa jambo analipata kwa Waziri Gwajima au idara ya habari, jambo ambalo ni zuri na muhimu sana katika upatikanaji wa taarifa kwa mujibu wa Sheria ya Upatikanaji Taarifa ya mwaka 2016.

Dk. Gwajima anaonekana kwenye jamii anashughulikia matatizo yanayogusa maisha ya watu. Anashiriki kuzuia hata kushughulikia taarifa za siri zinazotolewa na jamii na yuko kwenye makundi sogozi yenye wananchi wa kawaida kabisa wanaopinga ukatili na kote anapopokea taarifa fulani haraka anachukua hatua au kwenda kabisa mwenyewe.

Wakati mwingine jamii haihitaji hotuba ndefu pekee bali ni kwa kiasi gani unakuwa sehemu ya wanayopitia unatafuta majawabu.

Hivi sasa kuna kamati za kupinga ukatili kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa, ameelekeza masuala ya kijinsia kujadiliwa kwa uwazi kwenye kila kikao. Amewapa ujasiri wanawake kuhoji kuanzia kwenye mitaa yao na hajaacha kuwasema wale ambao hawatimizi wajibu na kuacha mambo yaharibike.

Kuonyesha upekee wa kiongozi huyu waandishi wa habari wamejumuishwa kwenye hizo kamati za kupinga ukatili wa aina yoyote kwenye jamii kwamba taarifa zinapatikana kwa urahisi zaidi na jamii inaelimishwa.

Mara kadhaa, mabalozi wa Umoja wa Ulaya (EU), ambao moja ya maeneo yao ni masuala ya wanawake na watoto, wameeleza kuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na nchi katika kuleta usawa wa kijinsia, huku wakieleza namna ambavyo Tanzania imekuwa mfano wa kuigwa Afrika kwa kuwa na mifumo inayofanya kazi.

Ukifuatilia utendaji kazi wa Gwajima, haujaanza sasa kwa sababu ni Waziri, bali alianza tangu akiwa mtumishi wa kawaida kabisa katika Hospitali ya Bagamoyo ambayo baadaye alikuwa kiongozi mkuu.

Baadaye alikuwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida. Nako aliendelea kuacha alama ya kutetea wanawake na watoto pamoja na Watanzania kwa ujumla, hata alivyokuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida.

Hakuishia hapo, alipokuwa Mkurugenzi Msaidizi, Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya aliacha alama ya kupaza sauti za wanyonge kwa muundo ule ule baadaye akawa Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI na Waziri wa Afya. Kote huko aliendelea kusikika kupigania haki za wengine bila kuchoka.


Jamii tumuunge mkono waziri na watendaji wake kufichua ukatili wa kijinsia kwenye jamii yetu. Wizara imepata kiongozi madhubuti ambaye anaijua jamii yake kuanzia ngazi ya kitongoji na mtaa, kinachotakiwa ni ushiriki madhubuti wa jamii ili ifike mahali tusema Tanzania hakuna ukatili.

Waziri huyu hatafikia lengo kama jamii itaendelea kulea ukatili, hivyo ni lazima kamati zifanye kazi, jamii itoe taarifa, mifumo ishirikiane na sheria ziendane na uhalisia.

Anaendelea kuonyesha kwa vitendo kwanini Rais aliona umuhimu wa kuwa na wizara hii na anaacha alama kwamba wizara hii ni muhimu,pia wanawake tunaweza.

**Mungu ibariki Tanzania.**








Msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Barnaba wakati akimvisha pete ya uchumba Raya Sykes katika  sherehe ya aina yake iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni







# MITINDO

## UBUNIFU WA UVAAJI

KATIKA suala la mavazi kwa mwanamke ni lazima awe anamiliki aina nyingi za nguo.

Kwa ujumla, matumizi ya nguo zaidi ya moja kwa wanawake ni jambo la kawaida katika kujiweka kwenye ubora.

Jambo la muhimu ni kuchagua aina tofauti ya nguo, ikiwa magauni ya mikono mirefu, mifupi au zinazovaliwa nyakati za joto na baridi.

Ikiwa una nguo za kutosha ndani ya nyumba, utakuwa na uhuru wa kuchagua na kuvaa nguo inayokwenda na wakati husika. Hii itakufanya kila siku kuwa tofauti na mvuto wa kipekee.

Unashauriwa kwenye mkusanyiko wako wa mavazi, epuka kuwa na nguo zitakazokufanya uonekane unakwenda kinyume na maadili ya jamii inayokuzunguka.


Pia jaribu kuchagua mavazi yanayolingana na mwili wako, hii itakufanya uonekane wa thamani na mwenye kujiamini.


Kwa wanaopenda kutaka kuonekana vizuri zaidi, ni vizuri kuwa na nguo zenye mpira katika mkusanyiko wako. Nguo zilizotengenezwa kwa mpira mara nyingi huleta ladha ya asili pale zinapovaliwa.

**Picha zote na Panterest**









UREMBO

Na Mary Geofrey

# TUNZA NYWELE NA DAWA

MARA nyingi tumekua tukiongelea nywele za asili lakini siyo watu wote wenye uvumilivu wa kutunza nywele kwa njia ya asili.

Nywele zinazokuzwa kwa dawa ni ambazo mwanzo zilikua za asili lakini zikaongezewa vilainishi ili kurudi kuwa katika hali bora na kuzifanya zikuwe kwa haraka.

Vitu vya kuzingatia

Hakikisha unachagua dawa inayoendana na nywele zako.

Hapa unatakiwa kutumia dawa zilizohifadhiwa katika pakiti ya boksi na sio za kopo, maana dawa za kopo ni kali zinaweza kuleta madhara ndani na nje ya kichwa kwa muda mfupi.

Na dawa za nywele zinawekwa chini tuu kwenye maotea ya nywele usiweke juu.

Dawa inatakiwa kuwekwa mara tatu au mbili tu kwa mwaka.

Kama nywele zako ni laini basi unaweka kila baada ya miezi sita na kama nywele zako ni ngumu basi kila baada ya miezi minne ndio unaweka.

Usiweke mara kwa mara, kumbuka hizo ni kemikali na zinaenda kukutana na ngozi ya kichwa moja kwa moja.

Panga kuweka dawa baada ya miezi mitatu vyote inategemea na aina ya nywele zako.

Wakati wa kusuka unashauriwa kutumia mitindo rafiki na nywele zako, usipende mtindo ambao utakata nywele zako.


Hakikisha unaosha nywele zako mara kwa mara, angalau mara tatu au nne kwa mwezi.

Nywele zikijaa uchafu haziwezi kupumua vizuri hivyo zitakua kwa kusuasua.

Tumia mafuta rafiki na nywele zako yenye uwezo wa kutunza unyevu na kuzuia kukatika.

Punguza matumizi ya moto kwenye nywele. Mfano kupasi nywele au kukausha nywele na dryer. Hii hufanya nywele kutokuwa na nguvu hivyo kuwa dhaifu sana hivyo unashauriwa usifanye mara kwa mara.

Tumia kofia ya satini au kitambaa cha safini wakati wa kulala. Hii inasaidia nywele kufyonza mafuta.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia tambi za mayai

MAPISHI ya tambi ni rahisi na yanatumia muda mfupi kuandaa, tofauti na vyakula vingine.

Chakula hiki hakichukui zaidi ya dakika 45 kuandaa.

Wakati mwingine mtu unakuwa umechoka na haupendi kupoteza muda jikoni, moja ya vyakula vya haraka ni tambi za mayai.

Mlo huu ni rahisi kuandaa na haukuchukui zaidi ya dakika ishirini chakula kinakuwa tayari mezani.

**MAHITAJI**

Tunahitaji vitu vichache tu na visivyo na gharama kutengeneza pishi letu.

Vitu hivyo ni pamoja na tambi, mayai na nyanya.

**NAMNA YA KUANDAA**

Ili kurahisisha na kutumia muda mchache jikoni unaweza kuanza kuchemsha maji huku ukiendelea na maandalizi ya viungo vingine.

Injika sufuria jikoni weka maji kiasi yatakayotosha kuchemsha tambi kisha ruhusu maji yachemke.

Saga nyanya zako vizuri kisha ukate vitunguu kwa mtindo unaopenda. Ukimaliza yote maji yako yatakuwa yamechemka.

Weka tambi ulizoziandaa kisha weka sukari vijiko vitatu vya chakula.

Kumbuka tunapika tambi nusu pakiti kwa kuwa mimi siwezi kumaliza mfuko wote.

Kama umepika pakti nzima, utakadiria kiasi cha sukari kadri ya mapenzi yako.

Kama sio mpenzi wa sukari unaweza kutumia chumvi kidogo. Acha tambi zako ziive huku ukiendelea kuandaa viungo vingine.

Andaa karoti kwa kuisaga, katakata hoho kwa maumbo mazuri yatakayovutia kwenye chakula. Hatua inayofuata ni kupasua mayai yako kwenye bakuli, weka chumvi kidogo na uyakorogoke vizuri kuchanganya chumvi na mayai.

Kama una majiko mawili itapendeza zaidi lakini ukiwa na moja hakijaharibika kitu. Tunaweza kutumia hilo hilo moja kufanya maajabu.

Anza kwa kutazama tambi zako kama zimeiva. Kama ndiyo, ziepue na uzitoe kwenye maji kama maji hayakukauka lakini kama maji yamekauka ziache humo humo kwenye sufuria.

Injika sufuria nyingine jikoni na uweke mafuta ya kupikia vijiko viwili au vitatu vya chakula, weka vitunguu maji kisha uvikaange mpaka viwe na rangi ya kahawia.

Vitunguu vikiwa tayari, kwenye sufuria hilo ongeza karoti yako uliyoisaga mapema na uikaange kwa muda wa dakika moja, ongeza nyanya kwenye mchanganyiko huo na uipike mpaka uanze kuona imeiva vizuri na mafuta yaonekane juu ya nyanya.

Weka mchanganyiko wa mayai na chumvi tuliouandaa kabla kisha ukoroge mpaka mayai yaive vizuri.



Baada ya hapo chukua tambi zako ulizochemsha na uongeze kwenye mchanganyiko wa vikorombwezo vyote.

Koroga vizuri ili tambi pamoja na vikorombwezo vyote vichanganyike vizuri, weka hoho na ufunike chakula chako kwa dakika nne tu.

Chakula chako kitakuwa tayari unaweza kufurahia mlo wako.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Panga ratiba ya usafi wa nyumba uiimarishe

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

**Mwingine** anaweza kusema mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka lakini ninachotaka kueleza ni kwamba ni namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuiimarisha na ikadumu zaidi. Kinyume chake, nyumba isiposafishwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo, ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.

Kwa mfano, kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba, hakikisha kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.

Kwenye maeneo yote ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiliwa, hakikisha unafanya hivyo. Kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama kila mahali pameguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Aidha, baada ya kusafisha hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndio utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.



## Namna ya kupamba saa ya ukutani



NYUMBA inapendeza kama ikiwa na mapambo yanayovutia, moja ya pambo muhimu ni saa ya ukutani.

Wakati wa kupamba kwa saa za ukutani ni muhimu kuwa na chaguo lako kama unapenda kuwa na saa halisi au zile za bandia.

Ni lazima kuwa na chaguo zuri la saa ndani ya nyumba ikiwamo aina, mitindo na kampuni iliyohusika kutengeneza.

Hizi ni baadhi ya dondoo muhimu za kufuata wakati unataka kupamba nyumba kwa saa ya ukutani.

**1: Saa ya kale**

Badala ya kuweka saa ya kawaida, ambayo inaweza kutambulika kwa sababu ni kitu tu cha kufanya kazi, tunaweza kuongeza saa nzuri ya zamani ukutani ambayo inatoa nakshi na ufanisi.

Kwa mfano, jikoni kama iko ya mtindo wa rustic, pia sebule ya kawaida au kwa mtindo mwingine kama Scandinavia.

**2: Saa kisasa**

Ikiwa unataka kuonekana wa kisasa zaidi, unaweza kuweka ukutani saa ya kisasa yenye mwonekano wa kushangaza. Hii itafanya nyumba yako kuonekana ni ya kisasa zaidi.

**3: Saa zilizochanganywa**

Wazo jingine zuri ni kuchanganya saa tofauti na za zamani kwenye kuta. Ni ngumu zaidi, na ikiwa tutatafuta saa za aina hii katika maduka ya mapambo, basi unaweza kupata vitu maalum vya kuchanganya.


Tafuta saa zenye ukubwa tofauti, rangi na maumbo na kisha ziweke ukutani kwa kila eneo linalostahili.

**4: Saa kubwa**

Kama unaweza kuweka saa kadhaa ndogo au za kati kwenye kuta zako, inawezekana pia kuweka saa kubwa ukutani.

Kipande ambacho kitavutia macho yote ni sebuleni na chumba cha chakula.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
HII MIDENI YOTE YA MIFAINI MAKOSA UNAFANYA SAA NGAPI?
HATA NAJUA BASI?
DALA - DALA
KESHO NITAENDESHA MWENYEWE
WE BABA NANIHII EMBU RUDI NDANI TUELEWANE KWANZA
SITAKI! NA UKIZIDI KUNISUMBUA NAENDA JOBU HIVI HIVI
NIMESIKIA DODOSO ETI NA WEWE ULIKUWA KALANI WA SENSA?
HELA NILOLIPWA ISHEISHA!
KUFANYAKAZI HII NI BASI TU! LAKINI MIMI NI MSOMI
RISIKIRIZENI HIRI... KWANI MTU AKIWAONA MRIVYOURAMBIA ATABISHA KAMA NYIE HAMJASOMA WOTE?
LABDA KASOMA NA MJOMBA'AKE LAKINI SIO MIMI
KWANI KOSA LETU NINI MBONA TUPO MUNKIDE? TUPO CHELEA PINA
SHOSTI MUMEO KAJA KUNICHUMBIA JANA MCHANA KWEUPEEE LEO ANANIOA
NIMEMSIKIA INATAKIWA DAMU YA MKEWE WA NDOA SIJUI YA NINI? NJOO TUTAJUA
GHARAMA YA MAISHA
LIKIKUGANDA USILINUNIE LIZOEE ILI LIKUZOEE
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...BILA KUKATISHWA TAMAA HUFIKI UENDAKO...



Wafungwa wakifunga makaburi wakati wa mazishi ya miili 70 ya wafungwa waliouawa katika ghasia katika makaburi ya Gereza la New Bilibid huko Muntinlupa, nchini Ufilipino. **PICHA: AFP**

# Mtoto wa rais wa Uganda aibuka na utata mwingine

**KAMPALA,** UGANDA

MTOTO wa rais wa Uganda, Jenerali Kainerugaba, ameibua mjadala kwenye mtandao wa Twitter baada ya kutuma ujumbe wenye utata alioambatanisha na picha ya zamani ya rais wa Rwanda, Paul Kagame.

Katika ujumbe huo, Jenerali Kainerugaba amesema wanaotaka kupigana na Rwanda ni sawa na kuanzisha vita na Uganda.

''Mimi ni Jenerali wa nyota nne wa UPDF,kuna vitu vichache ambavyo sijaviona katika dunia hii. Lakini ninawahurumia wale wanaomdharau mjomba wangu, Jenerali Kagame.

Kupigana na Rwanda inamaanisha kupigana na Uganda," ameandika Jenerali huyo.

Kauli hii inajiri huku mzozo kuhusu wapiganaji wa kundi la M23 ukiendelea kutokota kati ya Jamhuri ya kidemokrasi ya Congo na Rwanda.

DRC inaishutumu Rwanda kuwaunga mkono waasi wa M23 walioteka maeneo kadhaa mashariki mwa nchi hiyo, madai ambayo yanakanushwa.

Kwa upande mwingine Rwanda inaishutumu DRC kwa kushindwa kutimiza ahadi ya kuwarejesha nyumbani waasi wa Rwanda wa kundi la FDLR walioko mashariki inaowashutumu kuhatarisha usalama wa Rwanda.

Hivi karibuni pande mbili zilirushiana cheche za maneno, kila upande ukielezea uwezekano wa kuingia vitani iwapo usalama wake utayumbishwa.

Hali hiyo si mara ya kwanza kwa Jenerali Muhoozi, kutuma jumbe zenye utata kupitia mtandao wa kijamii kuhusu uhusiano wa nchi yake na nchi jirani, ambazo mara nyingi huibua gumzo mtandaoni.

Katika jumbe zake huwaelezea viongozi wa nchi jirani kama, makaka, na wajomba zake.

***BBC***

## Rais mteule wa Brazil kufanya ziara Marekani

**BRASILIA,** BRAZIL

RAIS mteule wa Brazil Luiz Inacio Lula da Silva na maofisa wa Marekani, wamesema kuwa kiongozi huyo anapanga safari ya kukutana na Rais Joe Biden katika Ikulu ya White House nchini Marekani.

Mkutano wa viongozi hao umepangwa kufanyika kabla ya kuchukua madaraka mnamo Januari 1 mwakani.

Msemaji wa baraza la usalama wa kitaifa la Ikulu ya White House John Kirby, aliwaambia wanahabari kwamba anaweza kuthibitisha mipango ya ziara hiyo.

Kirby aliongeza kuwa wanatazamia kumkaribisha Lula katika wakati mwafaka.

Aidha, Kirby alisema mshauri wa usalama wa taifa wa Biden, Jake Sullivan, atasafiri kuelekea Brazil siku ya Jumatatu kukutana na kundi la uongozi unaoingia madarakani wa Lula, pamoja na lile la utawala wa Rais anayeondoka Jair Bolsonaro.

Katika mkutano na wanahabari mjini Brasilia, Lula alisema kuwa yeye na Sullivan watafanya mazungumzo na kujadili kuhusu tarehe ya ziara hiyo.

Uwezekano wa ziara hiyo utakuwa baada ya Desemba 12 siku ambayo ushindi wake utaidhinishwa rasmi na jopo la uchaguzi la Brazil.

***DW***

# Nchi za Marekani na Ufaransa zaahidi kuibana Russia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MARAIS wa Marekani na Ufaransa wamesema wataiwajibisha Russia kwa matendo yake nchini Ukraine, huku Umoja wa Ulaya ukitangaza ukomo kwa bei ya mafuta ya nchi hiyo katika kuibania mapato ya kufadhili vita vyake.

Rais Joe Biden pia alisema atakuwa tayari kuzungumza moja kwa moja na Rais wa Russia, Vladmir Putin kuhusu kumaliza vita, lakini akaongeza kuwa hakuna dalili ya jambo hilo kutokea.

Mnamo Machi, mwezi mmoja baada ya kuanza kwa uvamizi, Biden alimuita Putin katili, kuhusiana na hatua zake na kusema kiongozi huyo hawezi kusalia madarakani.

Biden alisema baada ya mkutano wake na Macron mjini Washington, kwamba mataifa hayo pamoja na washirika watasimama kidete dhidi ya ukatili wa Russia.

"Tutaendeleza uungwaji mkono mkubwa kwa watu wa Ukraine wanapotetea makazi yao, familia zao, bustani zao, hospitali zao na uhuru wao wa mamlaka yao dhidi ya uvamizi wa Urusi," alisema Biden.

Alipoulizwa kuhusu kauli ya Rais wa Marekani Joe Biden kwamba atafanya mazungumzo na Putin, nchi yake itakapoondoka Ukraine, msemaji wa Kremlin Dymtri Peskov alisema kuwa Putin mara zote amekuwa tayari kwa mazungumzo, lakini matakwa ya rais Biden yatafanya mazungumzo kutowezekana.

"Rais wa Shirikisho la Russia amekuwa bado yuko tayari kwa mazungumzo ili kuhakikisha masilahi yetu. Rais alisema mazungumzo yanawezekana tu ikiwa Putin ataondoka Ukraine kwanza. Bila masharti, opereshni maalum ya kijeshi inaendelea." Alisema. Mapigano yameendelea kupamba moto mashariki mwa Ukraine, ambapo mji wa Bakhmut umekuwa shabaha ya mashambulizi ya makombora ya Russia, huku vikosi vya nchi hiyo katika mikoa ya kusini ya Kherson na Zaporizhzhia vikishambuliwa, kulingana na kamandi kuu ya jeshi la Ukraine.

Wakati huo huo, mmoja wa watu wenye ushawishi mkubwa wanaounga mkono uamuzi wa Rais Vladimir Putin, Yuri Kovalchuk, amesema kuwa vita inaweza kuonyesha uthabiti wa Russia kwa nchi za Magharibi . Bilionea Kovalchuk, aliyasema hayo katika makala ndefu ya jarida la Wall Street.

Nchini za Magharibi ni dhaifu na muda umefika kwa Russia kuonyesha nguvu zake za kijeshi kwa kuivamia Ukraine, alinukuliwa na vyanzo mbali mbali vya habari magazeti ya Marekani, akisema .

Mara kwa mara amekuwa akikutana na Putin kabla vita vya Ukraine havijaanza, na pia amekuwa akizungumza naye kwa njia ya simu na video.

Kovalchuk, ambaye aliwekewa vikwazo mwaka 2014, ni mfanyabiashara anayemiliki kampuni ya habari yenye vituo vya TV, magazeti, mitandao ya kijamii inayounga mkono serikali ya Russia. Wakati vita vya Ukraine vilipoanza, vyombo vyake vya habari vilikuwa muhimu kwa kueneza propaganda za utawala wa Russia, lilisema jarida la wall street.

***DW***

MAKALA

# KILA UHAI UNA THAMANI YAKE, TOKOMEZA UKATILI KIJINSIA



Na Magabilo Masambu

KILA uhai una thamani, tokomeza mauaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto". Hii ndiyo kaulimbiu ya mwaka 2022 kuhusu suala la kupinga ukatili wa kijinsia kwa kinamama na watoto. Kila ifikapo Novemba 25 kila mwaka, dunia inaadhimisha siku hii muhimu na siku 16 huwa zinatumika katika kutoa elimu juu ya masuala ya yanayochangia ukatili wa kijinsia.

Katika kutimiza azma hiyo, Novemba 25, mwaka huu, ulifanyika uzinduzi wa siku 16 za uanaharakati dhidi ya ukatili wa kijinsia uliofanyika katika viwanja vya Leaders' Club, Kinondoni. Mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye alipongeza wazo la msafara wa kupinga ukatili wa kijinsia kama njia nzuri ya kuifahamisha jamii kuhusu maadhimisho hayo.

Wadau, taasisi mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali yalishiriki katika uzinduzi huo. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam pia kilishiriki kuhakikisha kinaunga mkono juhudi za kupinga ukatili wa kijinsia, ikizingatiwa kwamba kimekuwa mstari wa mbele katika kutoa nafasi sawa kwa vijana wa kike na wa kiume katika kupata elimu ya juu.

Pamela Mollel, Waziri wa Jinsia na Watu Wenye Mahitaji Maalum katika Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DARUSO), alishauri kuwa pamoja na kwamba kampeni hii inahusu ukatili wa kijinsia kwa kinamama na watoto, kuna umuhimu mkubwa wa kutazama ukatili kwa watoto wa kiume na wanaume. Alisema kuna wanaume wanafanyiwa ukatili na wake zao, lakini wakati mwingine inakuwa ngumu kusema juu ya vitendo hivyo, kwa hiyo pia wanahitaji kusemewa.

Robert Makamba kutoka ofisi ya Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi chuoni, naye alisema kuna umuhimu wa jamii kwa ujumla kuanzia ngazi ya familia kuhakikisha amani inakuwa msingi wa maisha yao, ili kuepusha ukatili wa wanafamilia. Alisema kuna wakati ukatili huo unasababisha hata mauaji inapotokea migogoro ya kifamilia.

Kwa mujibu wa machapicho mbalimbali, inaelezwa kuwa chimbuko la maadhimisho haya yametokana na tamko la Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa awamu ya saba, Kofi Annan la mwaka 2006 la kutaka dunia itambue kuwa liko tatizo kubwa la ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wa kike, hivyo kuna umuhimu wa kuwa na kipindi maalum cha kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia ambayo ilikubalika ifanyike kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10 ya kila mwaka.

Lengo la kampeni hii ni kuongeza ushawishi, kubadilishana taarifa na uzoefu, kujenga uwezo wa pamoja, matumizi mazuri ya rasilimali zinazopatikana na kuunganisha nguvu za asasi za kijamii katika kuhamasisha, kuelimisha, kukemea na kuchukua hatua kwa pamoja ili kupinga ukatili wa kijinsia katika jamii.

Baada ya kusikiliza maoni ya baadhi ya watu, nami niseme kidogo. Kwanza, nakubaliana na hoja ya kupinga aina yoyote ya ukatili uwe amefanyiwa mwanamke, mwanamume au mtoto. Kupinga ukatili wa kijinsia katika makundi mawili pekee wakati karne ya leo tunazungumzia haki sawa pengine hatutaweza kuufikia usawa huo.

Ukatili wa kijinsia una sura nyingi. Uko ambao unatokana na tafsiri au unaotokea moja kwa moja. Huko duniani kuna baadhi ya nchi zimeweka zuio la baadhi ya watu hasa wanawake kutoshiriki katika baadhi ya mambo ya kijamii kama kutazama mpira, kuendesha magari, kutomiliki akaunti za benki na kadhalika. Inawezekana wao wenyewe wanaona ni jambo jema na wana sababu za kufanya hivyo, lakini kwa sisi tusiyo amini tutasema ni ukatili wa kijinsia.

Kuna ukatili wa kijinsia unaotokana na tafsiri ya mila na desturi za baadhi ya makabila. Mfano, kuna baadhi ya makabila mwanamke asipopigwa anaona kama hapendwi kwa sababu anahisi huna wivu naye na kwamba inawezekana una mwanamke mwingine. Sasa kitendo cha kumpiga kitatafsiriwa kama ukatili wa kijinsia.

Kuna ukatili wa kijinsia unaotokana na ukosefu wa elimu au umaskini, mfano baadhi ya jamii huwaozesha watoto wa kike wakiwa bado wadogo ambao wangetakiwa kuwa shuleni. Kundi hili la jamii linakosa elimu ya kufahamu umuhimu wa elimu kwa mabinti zao. Wanaona ni bora wachukue mahari kuliko kufikiria kwamba huyo binti akisoma akapata kazi, anaweza kununua mali nyingi zaidi kuliko mahari wanazopokea kwa ajili yake.

Uko ukatili unaotokana na uhusiano wa ndoa ndani ya familia. Hapa ziko sababu kadhaa na mara nyingi ni vigumu kujua mwenye matatizo au aliyetenda makosa kwa sababu mambo ya ndoa huendeshwa kwa usiri mkubwa. Kuna wakati anayeonekana anaonewa ndiye mwenye makosa na kuna wakati anakuwa ameonewa kweli. Kwa mila na desturi zetu, huwa ni rahisi jamii kuona mwanamke ndiye anaeonewa lakini kumbe ukifuatilia utagundua kwamba makosa hufanywa na wote.

ITAENDELEA WIKI IJAYO

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Wanamuziki hawataki mapenzi ya kusikiliza watu wa pembeni



Na Adam Fungamwango

MAPENZI ni ridhaa ya mtu mwenyewe kutamani au kumpenda mwingine. Hakuna yeyote anayelazimishwa au kushikiwa fimbo kupenda. Mapenzi huwa yanazuka tu na wala hayajulikani yametokea wapi.

Mtu anaweza kumpenda yeyote yule bila ya kuwa na kitu chochote kile ambacho kimemvutia. Yeyote anayempenda mtu kwa sababu ya kitu, basi penzi hilo lina matatizo. Siku kitu alichompendea kitatoweka, mapenzi yanakufa kifo cha asili. Mapenzi ni hisia tu. Mwanamume anaweza kuwaona wanawake hata 100, lakini akatokea mmoja akavutiwa naye. Na anayempenda atashindwa kuainisha ni nini haswa alichompendea. Anaweza kubabaisha tu, lakini ukweli kitu halisi kinakuwa nyuma ya ubongo wake.

Mwanamke naye anaweza kutongozwa na wanaume hata 100, akawakataa wote. Akatokea mmoja tu wa 101, akamkubali kwa sababu ambazo anaweza kuziainisha, lakini ukizifuatilia unaweza kukuta sifa hizo hata aliowakataa wanazo. Amemkubali kwa sababu ambazo hata yeye mwenyewe hazifahamu vizuri. Ni hisia tu. Kwa maana hiyo mapenzi ya mtu yapo kwa mtu mwenyewe. Ziko tabia za baadhi ya watu kujifanya walimu wa mapenzi ya watu. Si wanawake si wanaume.

"Kwa nini unampenda yule? Ana nini yule ambacho atakupa wewe? Maskini yule, hana kitu yule. Kwanza ana wanawake wengi, mimi mwenyewe ameshawahi kunitongoza nikamkataa."

Ni baadhi ya maneno ambayo hutoka kwa baadhi ya wanawake ambao hao kazi yao kuingilia hisia na mapenzi ya wenzao.

"Yaani ukimkubali nitakuona wewe hamna kitu kabisa shoga yangu, mkubali fulani, yule ana pesa, anakupenda na anakujali." Atampigia debe mwanaume mwingine ambaye labda humpa pesa kwa ajili ya kulainisha mambo. Asiye na msimamo anaweza kumkataa mwanamume anayempenda kwa sababu za kuambiwa na kuangukia kwa aliyelazimishwa kwa sababu ya matakwa au faida ya mtu mwingine.

Wanaume nao ni hivyo hivyo, baadhi yao wanatabia ya kwenda kwa wanawake na kuwalaumu kwa kupenda watu wengine.

"Yule atakwambia nini? Hana pesa, ana matatizo kibao, wewe tupende watu kama sisi." Hawa ni baadhi ya wanaume kwenye tabia hiyo. Kama mwanamke huna msimamo unaweza ukamwacha wako anayekupenda kwa dhati ukaangukia kwake ambaye hapendi ila anatamani tu.

Wako pia aina ya wafitini ambao wanawagombanisha hata watu walio kwenye ndoa. Ndoa nyingi zimevunjika kwa sababu ya watu wa aina hiyo na kuwaacha watoto wanateseka, hawasomi, wanahangaika na wengi wamekuwa ombaomba. Kisa maneno ya uongo ya kuambiwa. Ndiyo maana wanandoa na wapenzi siku zote wanaambiwa wasisikilize maneno ya pembeni, ni mabaya sasa.

Waamuzi wa penzi lao ni wao wenyewe. Walipopendana walikuwa wawili tu, iweje leo mtu wa tatu awe mwamuzi wa penzi? Kataa. Kupendana au kuachana iwe kwa sababu zenu wenyewe na si ushauri au maneno ya watu. Wanamuziki wa dansi wamekuwa wakishauri kwa miaka mingi kuhusu hilo.

Kwanza kabisa Amboni Jazz Band ya Tanga, wanamjia juu dada mmoja mmoja mwenye tabia ya kidomodomo kwenye mapenzi ya watu. Wakamwambia maneno haya kwenye wimbo waliouita 'Kidomidomi'.

"Wewe wajifanya wajua we dada. Unakuwa mwalimu wa wapenzi wa watu. Mimi nakukanywa, usiwe kidomidomi, utakuja adhirika ulimwenguni humu.

Usipende kashifu watu kwa wapenzi wao, utakuja adhirika dada mitaani, huko si kujenga dada ni kubomoa, mimi sikushauri kitu we dada endelea."

Ni wimbo uliokuwa na maneno mafupi, lakini yenye uzito mkubwa kwa watu wenye tabia kama hiyo. Maquis Du Zaire nao walikuwa na wimbo waliouita 'Mapenzi wa Mashahidi' ambao jamaa analalamikia mpenzi wake aliyekuwa anasikiliza maneno ya mtu wa pembeni ya dada mmoja anaitwa Asangamalembe aliyekuwa anamletea umbea.

"Tulipokutana mimi na we, hatukuwa na mashaidi, itakuwaje sasa mapenzi wamepiga hatua watuingilie. Ninavyosema mpenzi wangu unisikie, ninachotaka mimi na we tuishi mama kama zamani. Asangamalembe alifika nyumbani, kukupasha mambo ninayofanya, anachotaka mimi na wewe ahakikishe tumetengana.

"Asangamalembe, hataki tuishi mimi na we, Asangamalembe, alianza tangu zamani Asangamalembe. Asangamalembe kila siku nyumbani kwangu Asangamalembe. Asangamalembe, anachofuata mimi sielewi Asangamalembe, Asangamalembe ulisema shemeji yangu Asambamalembe, Asangamalembe, kazi yake kubwa umbea Asangamalembe."

Tubaki kwa hao hao Maquis, wakati huo sasa wakijiita Original walitoa wimbo unaitwa Nene. Mwanamke huyo hataki 'mbambamba'. Amewajia juu wale wote wanaomletea maneno ya uongo juu ya mpenzi wake mpya aliyempata.

"Kwa nini mtu apatapo mtu anayempenda, watu huanza chokochoko na maneno mengi. Wakati nilikuwa nikiishi peke yangu, wenzangu walinicheka mimi Nene, kwamba siolewi, sina mbele wala nyuma. Ulimwengu huu bahati ya mwenzio usiilalie mango wazi nasema yote haya huletwa na Mungu baba mimi Nene ukweli nasema.

Aliyenipenda kaamua mwenye kunipenda, amefurahi tabia yangu ananiita Nene. Uzuri wangu wa Tausi ni bahati yangu Nene, nimempata wangu 'cherie' (sherii) wa pete na

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.

Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HUYU mgonjwa pamoja na kwamba amepata nafuu sana na anakwenda kumalizia dawa na mguu amerudi kwenye hali yake ya kawaida mimi sitaki kwanza arudi nyumbani."

"Hata mimi nilikuwa na wazo kama hilo." Mumewe akadakia.

Mzee Mbegu akawatazama kwa zamu mtu na mkewe halafu akauliza "Kwa nini asirudi?"

Mama Vayajo akaangalia huku na huku kuona kama kuna mtu anasikiliza mazungumzo yao. Kumbuka walikuwa bado wodini. Walikuwa wanajiandaa kuondoka na mgonjwa aliyeruhusiwa. Lakini bado alikuwa amelala usingizi.

Alipoona hakuna mtu anayemuangalia akajibu "Kule ndiyo kuna wabaya wake, akirudi huyu anaweza kuumwa tena."

"Kuumwa tena na nyoka?" Mzee Mbegu akamuuliza mama mkwe wake.

"Hapana baba, ugonjwa unaweza kumrudia tena huyu." Akajibu.

"Mimi naona arudi tu kwa shangazi yake Morogoro." Baba wa mgonjwa akashauri, halafu akaongeza.

"Kwanza Kibaha si alikuja kwa muda tu? Arudi alikokuzoea."


"We baba Zulfa kwa hali hii. Yaani arudi Morogoro. Thubutu, labda mimi siyo mama yake. Mpaka nihakikishe mwanangu amepona kabisa."

Wote wakashtuka kwa msimamo wa mama huyo. Halafu ni kama macho yao yakawa yanamuuliza "Sasa unataka akakae wapi?"

"Nataka akaishi sehemu ambayo si mbali sana na nyumbani ili nipate hata nafasi ya mimi mwenyewe kumtazama mara kwa mara." Akajibu kana kwamba na yeye alijua swali atakaoulizwa baadaye.

"Wazazi wangu hebu naomba na mimi niongee. Samahani sana. Mimi nimejitolea tu matibabu na kila kitu, lakini sina mamlaka yoyote yale. Lakini naona nitoe ushauri tu."

"Sema tu mwanangu usiwe na wasiwasi." Baba Zulfa. Mpaka kufikia hatua hiyo, tayari Jerry alikuwa amejijengea heshima kubwa kwao. Kitendo cha kukimbiwa na mke siku ya harusi, lakini bado amekuwa karibu na familia katika kipindi cha kumuugusa shemeji yake, huku akijitolea gharama za matibabu, zilimfanya kukubalika mara dufu.




**"Wazazi wangu hebu naomba na mimi niongee. Samahani sana. Mimi nimejitolea tu matibabu na kila kitu, lakini sina mamlaka yoyote yale. Lakini naona nitoe ushauri tu."**

"Naomba kama itawapendeza Zulfa akae kwangu kwa muda wakati anarudisha afya yake."

Kimya kilitawala. Haikujulikana kama hawajaafiki au wanatafakari. Mzee Mbegu akaamua kuvunja ukimya wa sekunde chache.

"Mimi sioni vibaya kwa hilo."

"Kama kuna usalama sawa." Baba Zulfa naye alijibu kwa sauti ambayo ilionekana kama ana mashaka fulani hivi.

Jerry alimuelewa baba mkwe wake akajibu.

"Mzee nyumbani kwangu hakuna wasiwasi. Kuna usalama nadhani kushinda usalama wenyewe." Akajibu kwa msisitizo.

Jerry alimuelewa mkwewe usalama anaousema ni kuwa kama hakuna mwanamke mwenye uhusiano wowote kwake kwa wakati huo, kwani isingekuwa rahisi binti yao kuishi kwa usalama huko chini ya mtu mwingine, huku akijua hana uhusiano wowote zaidi ya ushemeji tu. Tena kwa mwanamke ambaye alimkimbia mwanaume siku ya harusi.

"Mimi sina neno mkwe wangu, tumsubiri mgonjwa mwenyewe aamke, akikubali hata mimi sina tatizo. Umetusaidia sana na bado unataka kuendelea kutusaidia. Mungu akuongezee baba, una moyo hasa, umetoka kwenye mifupa ya watu. Sahau yaliyopita baba." Yalikuwa ni maneno ya mama Zulfa.

Dakika 10 baadaye Zulfa aliamka. Baada ya dakika tano za kukaa sawa na kuongea na waliomtembelea hospitali, mama yake alimuuliza swali hilo.

"Kwenda kukaa kwa shemeji Jerry, hakuna tatizo." Hakuna yoyote aliyetarajia kama Zulfa atakataa. Hata yeye alijua hali aliyonayo kwa sasa ni juhudi kubwa zilizofanywa na shemeji yake huyo.

"Haya babu kazi kwako." Mzee Mbegu akamnong'oneza Jerry, wakaangua vicheko wote wawili wakiwaacha wengine wasijue nini kinazungumzwa, lakini hawakutaka kuuliza kitu chochote kwani wanafahamu kuwa watu hao wanaelewana na kupendana sana, mtu na babu yake.

****************************************

Ilikuwa ni mapema mno kuliko ilivyotarajiwa. Mwezi mmoja tu baadaye afya ya Zulfa ilionekana kuimarika kuliko ilivyotegemewa na yeyote yule. Hata baba na mama yake ambao walikuwa wakienda mara kwa mara nyumbani kwa Jerry baadaye hawakuona sasa umuhimu huo, kwani kila siku zilivyozidi kusonga mbele si tu kwamba alionekana anapona, lakini ananawiri.

Uzuri na urembo wake ulikuwa mara mbili au tatu ya alivyokuwa mwanzo. Nyumbani kwa Jerry alikuwa akisaidiwa zaidi na msichana wa kazi.

Kazi ya Jerry siku zote ilikuwa ni kuongea naye anaporejea kutoka kazini, kumpa faraja, ili kumuweka sawa kisaikolojia kwani kuna wakati ugonjwa ulimsababisha akate tamaa ya kuishi.

"Unajua nilikata tamaa kabisa." Zulfa alisema akiwa anatafuna bisi, akishushia na juisi. Walikuwa wamekaa sebuleni pamoja na msichana wao wa kazi wakiangalia tamthilia.

Muda wote akiishi hapo, Zulfa alikuwa akilala na msichana wa kazi, Jerry akilala kwenye chumba cha peke yake.

Mwanzoni alipofika alipowaambia jirani zake na watu wengine kuwa ni mgonjwa wake anamtunza hapo waliamini. Lakini kwa jinsi alivyo sasa, akiwa na uwezo wa kutembea vizuri kiasi cha kuweza kutoka pamoja kufanya mazoezi ya kutembea kama alivyoambiwa hospitalini, hao hao wanakataa, wanadai ni mpenzi wake.

"Kwani ulijua utakufa?" "Ndiyo."

"Hivi unadhani binadamu anakufa kirahisi namna ile?"

Zulfa akageuza shingo, akamtazama Jerry usoni. "Una maana gani shem Jerry?" "Au na wewe unaungana na mama yako kwamba ulirogwa?" "Mmmh, mimi siamini sana, lakini dunia hii ina mambo wewe."

"Hivi ni kweli kuna kijana anaitwa Said alikuwa anakutaka?" Maswali yalizidi kumiminika kutoka mdomoni mwa Jerry. "We nani kakwambia?" "Babu mzee Mbegu." Zulfa akaangua kicheko cha aina yake. Ni kicheko cha umbea hivi.

"Babu naye kumbe mmbea hivi, kakwambiaje?"

"Jibu kwanza swali langu Zulfa usilikwepe." Jerry akamkazia macho huku akitabasamu. "Huo ndiyo mzozo wenyewe. Yule kijana nilimkataa, eti alitaka anioe, kaanza kuwaambia wazazi wake, ndugu zake kabla hata hajaniambia, nikamwambia aka babu nipishe mie, aliyekwambia nina shida ya mwanaume nani? Aliyekuambia ana shida ya kuolewa nani? Ila aliumia sikufichi. Kaumia sana.

**ITAENDELEA JUMAPILI**




# TICHA STAR KUWANIA TUZO ZA MUZIKI WA DANSI

MSANII wa muziki wa dansi wa kizazi kipya, ajulikanaye kwa jina la Ticha star, ameteuliwa kuwania tuzo za muziki wa dansi zitakazotolewa nchini.

Sherehe ya utoaji wa tuzo hizo zinazojulikana 'Cheza Kidansi Music Award' na kuratibiwa na kampuni ya Cheza Kidansi, itafanyika usiku wa Desemba 9, katika ukumbi wa Break Point jijini Dar es Dalaam.

Ticha star mwenye makazi yake jijini Dodoma, ameteuliwa kuwania katika vipengele viwili, ambavyo ni Mwanamuziki bora chipukizi na Wimbo bora wa kushirikiana na msanii mwenzake.

Akizungumza na Nipashe, Ticha star amewaomba watanzania wampigie kura nyingi kupitia HYPERLINK "http://www.chezakidansi.com/" \t "_blank" www.chezakidansi.com.

Ili kuweza kumpigia kura, unaingia kwenye tovuti hiyo na kwenda kipengele chenye jina la Ticha star, unabonyeza pembeni na kisha unabonyeza sehemu iliyoandikwa "PIGA KURA".

Katika tamasha hilo ambalo litapambwa na burudani kibao kutoka kwa wanamuziki maarufu, kiingilio kitakuwa shilingi 10,000 kwa kila mtu.

# *Bila mil.100 kolabo na Harmonize hakuna*

WASANII wa Bongo wanaotaka kolabo na Harmonize, wanatakiwa kujichanga sana, kwani bila kuwa na shilingi milioni 100, unatakiwa kukaa pembeni.

Harmonize kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameweka wazi kwamba hata kama una kitita hicho cha pesa, bado unatakiwa kufuata kigezo kingine cha nyimbo yako kama ni kali au la.

Amesema endapo kuna msanii ambaye anajiona amekidhi vigezo hiyo, yuko tayari kufanya naye



## ZISIKUPITE

### MADRID YARUDI KWA MBAPPE

KLABU ya Real Madrid itakuwa bado inataka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23 kutoka Paris St-Germain, lakini kama tu masharti fulani yatatimizwa . (***Sport, via 90 Min***)

### LEWANDOWSKI ALITAKIWA PSG

KYLIAN Mbappe alikutana na Robert Lewandowski katika msimu wa joto katika azma ya kumshawishi mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Poland mwenye miaka 34 kujiunga naye PSG badala ya kusaini mkataba na Barcelona. (***Le Parisien***)

### NKUNKU KUTUA CHELSEA

CHELSEA italipa euro milioni 70 kumsajili mshambuliaji, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 25 kutoka RB Leipzig. (***Nicolo Schira***)

### RONALDO AITAZAMA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 ana 'shawishika sana ' kuhusu kujiunga na Chelsea baada ya kuondoka Manchester United. (***Calciomercato, via Express***)

### DAVID AITAMANI EPL

MSHAMBULIAJI wa Lille na Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David mwenye miaka 22, amekiri kucheza Ligi Kuu England maarufu EPL, imeendelea kuwa ndoto yake. ***(Independent)***

### CHAVEZ ANUKIA LEVERKUSEN

KLABU ya Bayer Leverkusen imekuwa katika mkataba na Club Pachuca juu ya uwezekano wa uhamisho wa Luis Chavez baada ya kufurahishwa na kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 26 katika Kombe la Dunia. ***(90 Min)***

### HAZARD KUSTAAFU UBELGIJI

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Eden Hazard anaangalia uwezekano wa kustaafu soka la kimataifa akiwa na umri wa miaka 31 baada ya kuondolewa mapema kwa Ubelgiji katika mashindano ya Kombe la Dunia. ***(Marca)***

### SOYUNCE ATAJWA ROMA

AS Roma inafikiria kumnunua mlinzi wa Leicester City na Timu ya Taifa ya Uturuki, Caglar Soyuncu mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha dogo la Januari. (***Calciomercato***)

### CHELSEA YAMGOMEA PULISIC

CHELSEA haiko tayari kumruhusu winga wa Marekani, Christian Pulisic, kuondoka kwa mkataba wa mkopo Januari na wangependelea uhamisho wa kudumu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (***Mail***)

### FOFANA KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imeanza mazungumzo na Molde ya Norway ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye miaka 19. (***Fabrizio Romano***)

### LAIMER, BAYERN SAFI

BAYERN Munich inaamini imekamilisha makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Austria, Konrad Laimer, mwenye umri wa miaka 25. (***90min***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TITE ATAHADHARISHA WAKO HATUA NGUMU

## ●●● Aeleza wanahitaji kuendelea kujituma zaidi ili kupata matokeo chanya kwa...

**DOHA, Qatar**

KOCHA Tite ameonya Brazil lazima iwe "makini sana" katika hatua ya mtoano ya Kombe la Dunia, wakati watakuwa na matumaini ya kumrejesha Neymar kutoka kwenye majeruhi.

Selecao hao walifungwa bao 1-0 na Cameroon katika mechi iliyochezwa juzi lakini bado wanaongoza Kundi G, inamaanisha watamenyana na Korea Kusini katika raundi ya pili.

Kichapo cha Hispania siku iliyotangulia kilionekana kufungua droo zaidi kwa Brazil, ambayo sasa itacheza na mshindi wa pambano la Japan na Croatia katika robo-fainali.

Bila kujali wapinzani wao, Brazil watajisikia raha zaidi Neymar atakaporejea uwanjani, lakini bado hajafanya mazoezi.

> **Daktari wa timu, Rodrigo Lasmar alisema: "Kwa saa 72 kabla ya mechi in ayofuata, tuna wakati upande wetu. Bado tu nao uwezekano."**

Akiwa na nyota wake au bila nyota wake, Tite hakika hataridhika, akieleza: "Brazil ilishindwa na Cameroon. Ureno ilishindwa na Korea Kusini. Ufaransa ilishindwa na Tunisia. Argentina ilishindwa na Saudi Arabia. Nadhani matokeo yanajieleza yenyewe.

"Nadhani hizi ni mechi kali sana, ngumu sana. Sidhani tunaweza kufikiria hali yoyote ya hapo awali inafanya iwe rahisi. Tunahitaji kuwa waangalifu sana.

"Tulikuwa makini sana na mechi dhidi ya Cameroon. Tulikuwa na wasiwasi wote, tukawachukua. Walikuwa na sifa zao, walicheza vyema sana. Wana sifa ya ushindi kama Tunisia na wengine.

"Hatuwezi kusema ni rahisi na tuna faida. Hatuwezi kusema hivyo."

"Nani alipoteza? Sisi sote. Maandalizi yetu ni maandalizi ya pamoja, ushindi wetu ni ushindi wa pamoja, hasara zetu pia ni hasara za pamoja."

Kocha huyo alitoa wito kwa Brazil "kuhisi kupoteza", akisema: "Kombe la Dunia halikupi nafasi ya pili.

"Tunapaswa kuzingatia kwa saa 24, kuteseka kwa saa 24, na kesho (jana)tunaanza kujiandaa."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

ENGLAND
VERSUS
SENEGAL

1 | 1.58
X | 3.61
2 | 6.28

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# XHAKA KATIKA HATIHATI YA KUFUNGIWA NA FIFA

**DOHA,** Qatar

GRANIT Xhaka alijikuta katikati ya mzozo mwingine uliohusisha Serbia kwa kuvaa jezi yenye jina 'Jashari' mgongoni baada ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Uswisi katika mechi iliyochezwa mjini Doha hapo juzi.

Xhaka aliibuka mchezaji bora wa mechi hiyo wakati ambapo timu yake ilitoka nyuma kwa mabao 2-1 na kujihakikishia nafasi ya pili kwenye Kundi G na kutinga hatua ya 16, watacheza na Ureno keshokutwa.

Lakini matendo yake baada ya kipenga cha mwisho yanaweza kuvutia hisia za FIFA.

Katika sherehe za baada ya mechi, Xhaka alivaa jezi iliyokuwa na jina la 'Jashari'.

Alipoulizwa baadaye nini maana yake, kiungo huyo wa kati wa Arsenal alidai ni kiungo wa kikosi cha Uswisi, Ardon Jashari.

Hata hivyo, jina hilo lina umuhimu kwa njia nyinginezo kwani, Adem Jashari ni mwanzilishi wa Jeshi la Ukombozi la Kosovo, Kundi la Waalbania lililopigania uhuru kutoka kwa Yugoslavia ya zamani.

Xhaka ana asili ya Albania iliyohusishwa na Kosovo, ambayo ilitangaza uhuru wake mwaka wa 2008, lakini haijatambuliwa na Serbia.

Alipoulizwa kuhusu jezi hiyo, Xhaka alisema: "Hakuna historia yoyote ya kisiasa.

"Ardon ni sehemu ya kikosi chetu na tunatumia muda mwingi pamoja. Nilimwambia iwapo tutashinda nitavaa jezi yake."

# Rigobert: Cameroon tumeumia

**DOHA,** Qatar

RIGOBERT Song alielezea masikitiko yake baada ya Cameroon kuondolewa kwenye Kombe la Dunia licha ya kuwa timu ya kwanza ya Afrika kuifunga Brazil kwenye michuano hiyo.

Cameroon ilihitaji ushindi ili kutinga hatua ya 16 bora siku ya Ijumaa, na walifanya hivyo kwa namna ya kushangaza huku Vincent Aboubakar akifunga bao pekee la ushindi kabla ya kuonyeshwa kadi ya pili ya njano iliyozaa nyekundu kwa kuvua jezi.

Hata hivyo, ushindi wa kusisimua wa 3-2 wa Uswizi dhidi ya Serbia uliwafanya Cameroon wakose nafasi ya kutinga hatua ya 16 bora.

Simba hao wasiofugika angalau walifanya vyema kwa kuhitimisha rekodi kamili ya Brazil katika Kombe la Dunia dhidi ya timu za Afrika (hapo awali walicheza saba, wakashinda saba), lakini Song alihisi matokeo yalionyesha Cameroon wangeweza kwenda mbali zaidi.

"Sikujua hata huu ulikuwa ushindi wa kihistoria. Sisi ni moja ya nchi za Afrika ambazo zimecheza Kombe la Dunia zaidi kuliko nyingine, na sasa tumeishinda Brazil," alisema Song.

"Wachezaji wangu wanastahili kupongezwa. Walionyesha usiku wa leo (juzi) wangeweza kufanya vizuri zaidi.

"Nadhani tuna hisia ya majuto. Sasa tunatambua tungeweza kufanya vizuri zaidi. Lakini tunahitaji kuangalia upande mzuri pia.

"Ninajaribu kupata ari ya timu, roho ya simba, ambayo inapaswa kuwa ufunguo wa timu za Cameroon.



## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI – 04/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1098 | Kapaz vs FK Sumgayit | 2.17 | 3.30 | 3.25 |
| 13:30 | 4467 | Manisa BBSK vs Keciorengucu | 2.14 | 3.45 | 2.92 |
| 14:00 | 3796 | Kenkre FC vs Gokulam Kerala FC | 5.46 | 3.80 | 1.53 |
| 14:00 | 3882 | Numancia vs Real Union Irun | 1.69 | 3.41 | 4.68 |
| 14:15 | 3506 | Farul Constanta vs Botosani | 1.66 | 3.66 | 4.85 |
| 14:30 | 1047 | Spal vs Modena | 2.31 | 3.07 | 3.12 |
| 15:00 | 2193 | MTK Budapest vs Gyirmot FC | 1.83 | 3.79 | 3.45 |
| 15:00 | 2380 | Csakvari TK vs FC Gyori Eto | 2.19 | 3.21 | 3.02 |
| 15:00 | 2936 | Mosonmagyarovar vs Soroksar | 2.31 | 3.41 | 2.68 |
| 15:00 | 4366 | Dorogi FC vs Pecs MFC | 4.57 | 3.30 | 1.73 |
| 15:30 | 2482 | Kalamata FC vs Episkopi FC | 1.21 | 5.06 | 13.62 |
| 15:30 | 3731 | Wycombe vs Portsmouth | 2.39 | 3.32 | 2.78 |
| 15:30 | 4970 | Omonia Aradippou vs AEZ Zakakiou | 2.17 | 3.25 | 3.35 |
| 16:00 | 1044 | Mosta vs Zebbug Rangers | 1.85 | 3.46 | 3.70 |
| 16:00 | 1276 | FC Andorra vs FC Cartagena | 2.20 | 3.03 | 3.38 |
| 16:00 | 2480 | Lokomotive Leipzig vs Chemnitz | 2.42 | 3.45 | 2.52 |
| 16:00 | 2849 | AE Larissa vs Thesprotos | 1.28 | 5.00 | 11.00 |
| 16:00 | 4586 | Zira vs Turan Tovuz | 1.94 | 3.36 | 3.50 |
| 16:00 | 4921 | Proodeftiki FC vs Kifisias | 6.02 | 3.40 | 1.56 |
| 16:00 | 5652 | Adanaspor vs Goeztepe | 2.57 | 3.25 | 2.48 |
| 16:00 | 5868 | Valletta vs Gudja United | 2.07 | 3.40 | 3.40 |
| 16:30 | 3610 | Pro Vercelli vs Pordenone | 3.75 | 3.20 | 2.04 |
| 16:30 | 4452 | CFR Cluj vs Chindia Targoviste | 1.67 | 3.47 | 5.15 |
| 16:30 | 5340 | Vicenza vs US Pergolettese | 1.79 | 3.45 | 4.50 |
| 17:00 | 1162 | Genoa vs Cittadella | 1.57 | 3.67 | 5.94 |
| 17:00 | 1212 | Sudtirol vs Frosinone | 3.32 | 2.97 | 2.26 |
| 17:00 | 1465 | Newry City AFC vs Portadown FC | 1.46 | 4.19 | 5.65 |
| 17:00 | 2066 | Brescia vs Reggina | 2.50 | 2.94 | 2.94 |
| 17:00 | 2388 | Ascoli vs Como | 2.07 | 3.26 | 3.46 |
| 17:00 | 3473 | Liverpool W vs West Ham W | 2.42 | 3.70 | 2.41 |
| 17:00 | 4370 | Bari vs Pisa | 2.10 | 3.17 | 3.47 |
| 17:00 | 4378 | Jamshedpur vs Kerala Blasters FC | 2.36 | 3.25 | 2.72 |
| 17:00 | 5272 | Cosenza vs Perugia | 2.88 | 3.03 | 2.48 |
| 18:00 | 2056 | France vs Poland | 1.27 | 5.20 | 11.01 |
| 18:00 | 3884 | Anorthosis Famagusta vs Aris Limassol | 3.00 | 3.25 | 2.33 |
| 18:15 | 3770 | Racing Santander vs Lugo | 1.76 | 3.43 | 4.57 |
| 18:30 | 1960 | Olot vs Hercules CF | 2.91 | 2.77 | 2.53 |
| 19:00 | 3219 | Altay vs Boluspor | 4.18 | 3.25 | 1.81 |
| 19:30 | 2185 | Monopoli vs Potenza SC | 2.10 | 3.21 | 3.56 |
| 19:30 | 3586 | Fidelis Andria vs Juve Stabia | 2.71 | 2.91 | 2.81 |
| 20:00 | 1831 | Gimnastic Tarragona vs CE Sabadell | 2.02 | 3.07 | 3.60 |
| 20:00 | 2510 | Benevento vs Palermo | 1.96 | 3.22 | 3.86 |
| 20:00 | 3158 | Argesul Pitesti vs Rapid Bucuresti | 4.05 | 3.36 | 1.87 |
| 20:00 | 4837 | Apollon Limassol vs AEL Limassol | 2.09 | 3.24 | 3.54 |
| 20:00 | 4892 | FC Arouca vs Leixoes | 1.88 | 3.35 | 3.69 |
| 20:00 | 5642 | MSK Deinze vs RS Waasland Beveren | 3.25 | 3.70 | 1.97 |
| 20:30 | 5872 | Eibar vs Huesca | 1.79 | 3.27 | 4.66 |
| 22:00 | 4851 | Alverca Futebol vs CF Os Belenenses | 2.03 | 3.11 | 3.50 |
| 22:00 | 4950 | England vs Senegal | 1.58 | 3.61 | 6.28 |
| 23:00 | 2651 | Levante vs Malaga | 1.60 | 3.67 | 5.55 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KVZ YAAHIDI KUJIIMARISHA IKITAMBA NA UNBEATEN 15

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Dulla Boys, KVZ imekuwa ndio timu pekee ambayo haijapoteza mechi hata moja katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar wenye michezo 15, imefahamika.

Maafande hao wa KVZ katika michezo hiyo 15 wameshinda mechi nane na kutoka sare michezo saba na kujikusanyia pointi 31 zinazowaweka kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) huku wapinzani wao wakuu wakiwa ni Malindi yenye pointi 28 ikiwa katika nafasi ya pili.

Kocha Msaidizi wa KVZ, Ali Khalid, alisema wanaenda mapumziko ya dirisha dogo wakiwa na malengo ya kukiimarisha kikosi chao kwa sababu wanataka kutimiza malengo waliyojiwekea.

"Kila timu inayowania ubingwa lazima iende ikafanye maandalizi ya kuongeza nguvu katika kikosi chake ili mzunguko wa mapambano unapoanza kila mmoja hataki kufanya makosa," alisema Khalid.

Kocha huyo alisema anahitaji kupata mafanikio zaidi kwa sababu malengo yake ni kuona wanatwaa ubingwa wa msimu huu.

"Tumemaliza mzunguko wa kwanza tukiwa "Unbeatean", hii haina maana ndio tubweteke, hapana tunahitaji kutumia mapumziko haya kwa ajili ya kujiimarisha kuboresha timu yetu, najua mzunguko wa mapambano ukifika kila mmoja anaangalia mbele katika kufikia malengo yake, hivyo na sisi tunaenda kujipanga," aliongeza kocha huyo.

Wakati huo huo Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza dirisha dogo la usajili na uhamisho wa wachezaji litafunguliwa rasmi ifikapo Desemba 13, mwaka huu na litafungwa ifikapo Januari 12, mwakani.



Mwenyekiti mpya wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dar es Salaam, Abbas Mtemvu (katikati), akicheza muziki wakati alipopokelewa katika Ofisi ya chama hicho mapema wiki hii. Wengine ni viongozi wa CCM jijini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Simba yarejea kileleni kibabe*

INATOKA UK 24

Kitabu cha mabao kwa Simba kilifungwa dakika mbili kabla ya mechi kumalizika kupitia kwa Chama, akifunga bao kwa mpira ambao ulidondoka mbele yake na kuusukuma ndani ya vyavu.

Ilikuwa ni baada ya hekaheka nzito iliyofanywa na Phiri aliachia kombora kali lililopanguliwa na Mroivili ukarejea ndani, ukamkuta Bocco ambaye alipiga kichwa mpira ukagonga mwamba wa juu na kutua chini kabla mfungaji hajaumalizia.

Dakika chache kabla mechi kumalizika, kiungo mkabaji wa Simba, Sadio Kanoute, alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa mchezo mbaya, ikiwa ni kadi ya pili ya njano.

Kwa matokeo hayo, Coastal Union imeshuka hadi nafasi ya 13, ikiwa na pointi 12 kibindoni.

## Mayele hatihati kuikabili Prisons

INATOKA UK 24

"Tunawakosa Mayele, Job na Moloko, lakini tayari kuna baadhi ya wachezaji wamerejea kikosini akiwamo Farid Mussa, Djuma Shabaan na Bernard Morrison, tayari wamefanya mazoezi mepesi," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Naye Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaban Mtupa, alisema wamefanya maandalizi mazuri kwa kurekebisha mapungufu yao kwa ajili ya kuhakikisha wanavuna pointi zote kutoka kwa Yanga.

"Tuko tayari kukutana na Yanga kwa lengo moja la kuvuna pointi tatu, hatuwaogopi bali tunawaheshimu, tunajua wapinzani wetu wako vizuri, lakini kwa upande wetu pia tumewaanda vyema kisaikolojia wachezaji wetu. Kulikuwa na shida katika eneo la ushambuliaji ambalo tayari tumelifanyia kazi, kwa kutumia madhaifu ya Yanga basi tutaondoka na pointi tatu, wapinzani wetu wanafungika ," alisema Mtupa.

Nahodha wa Prisons, Benjamin Asukile, alisema licha ya ahadi waliopewa na mdhamini wao ya kupata Sh. milioni 20 endapo watashinda, wao wanaangalia zaidi kupata pointi ili kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

"Watu wa Mbeya wametutuma kuja kufanya kazi, tutahakikisha tunatimiza kile kilichotuleta Dar es Salaam, tutaendelea pale waliipoishia wenzetu (Ihefu FC), tuko tayari kwa mapambano," aliongeza nahodha huyo.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Polisi Tanzania kuwakaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa Ushirika ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro.

# Michezo

Jumapili Desemba 4, 2022

Nipashe



Tite atahadharisha wako hatua ngumu

UKURASA 21



Kiungo wa kimataifa wa Simba, Clatous Chama (kushoto), akijipanga kumtoka beki wa Coastal Union, Albano Mtenje (kulia) katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Mayele hatihati kuikabili Prisons

**Na Saada Akida**

IKIWA katika hatihati ya kumkosa mshambuliaji wake nyota, Fiston Mayele, kikosi cha Yanga kinatarajia kuikaribisha Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nyota wengine ambao Yanga itakawakosa katika mechi hiyo ni Dickson Job, Jesus Moloko kutokana na majeruhi waliyonayo lakini pia kocha wao mkuu, Nesreddine Nabi, ambaye amefungiwa mechi tatu. Kamati ya Uendeshaji ya Ligi Kuu Tanzania Bara imemfungia Nabi pamoja na kumtoza faini ya Sh. 500,00 baada ya kukutwa na hatia ya kuwashambulia waamuzi kwa maneno wakati Yanga ilipokuwa ugenini Mbarali kucheza dhidi ya Ihefu SC.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wanatambua mchezo utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao.

Kaze alisema wamezungumza na wachezaji wao na kuwataka wasahau matokeo ya mechi iliyopita na sasa waingie na mawazo mapya kwa ajili ya kusaka alama tatu huku wakifahamu Prisons ina kikosi imara.

"Tunafahamu kutafuta pointi tatu ni daraja kubwa katika ligi, tumepoteza mechi iliyopita na timu kutoka Mbeya, na kesho (leo), tutacheza na timu nyingine kutoka mkoa huo huo, ila ni timu tofauti na sisi tumejipanga vizuri kwa sababu tunacheza nyumbani," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema kukosekana kwa baadhi ya wachezaji wao nyota haiwafanyi wawe na hofu, anaamini nyota wengine waliobakia watapambana ili kufikia malengo ya klabu.

INAENDELEA UK 23

# Simba yarejea kileleni kibabe

## ●●● Yaichapa Coastal Union 3-0, Phiri akimkamata Mayele katika mbio...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO yaliyofungwa na wachezaji wawili raia wa Zambia, Mosses Phiri na Clatous Chama wa Simba katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, Tanga jana yalimpaisha Mnyama hadi kileleni.

**Phiri alifunga mabao mawili, akifikisha magoli 10 kwenye orodha ya wafungaji wa ligi hiyo sawa na Fiston Mayele wa Yanga, huku Chama akifunga moja na kutoa pasi ya mwisho kwenye bao moja.**

Ni matokeo ambayo yameifanya Simba ifikishe pointi 34, ikimaliza mzunguko wa kwanza kwa kuzifumania nyavu za wapinzani mara 31, lakini ikiruhusu mabao saba kutinga wavuni katika lango lao.

Mabao yote ya Simba katika mechi hiyo iliyochezeshwa na mwamuzi, Jonesia Rukyaa kutoka Kagera yalifungwa kipindi cha pili baada ya kubanwa mbavu dakika 45 za kwanza, huku wachezaji wakionekana kutochangamka ukilinganisha na kasi waliyoionyesha kipindi cha pili.

Simba ingeweza kupata bao la kuongoza dakika ya tisa tu ya mchezo kama mpira uliopigwa kwa kisigino na beki, Henock Inonga, usingetoka nje kidogo ya lango la Coastal Union, mchezaji huyo alipiga mpira huo baada ya kupata pasi ya kichwa kutoka kwa nahodha, John Bocco, kutokana na faulo iliyopigwa na Chama.

Dakika tatu baadaye Bocco kama angekuwa makini angeweza kuipatia timu yake bao, kwani alipata mpira akiwa kwenye eneo zuri, lakini alionekana kubabaika na kuupiga vibaya mpira uliotoka pembeni ya lango la wenyeji.

Inonga alikosea kuumiliki mpira, akanyang'anywa na kijana mwenye kasi, Hamad Majimengi, ambaye alimwacha na kuelekea kwenye lango la Simba, lakini alikuwa mchoyo akataka kupiga mwenyewe shuti badala ya kupiga krosi kwa wenzake, mpira ukaambaa nje ya lango.

Golikipa chaguo la kwanza wa Simba, Aishi Manula, alilazimika kuruka juu na kupangua shuti kali la mbali lililopigwa na Vicent Aboubakar dakika ya 19 na kuinyima Coastal Union nafasi ya kufunga bao, hata hivyo mchezaji huyo hakurejea kipindi cha pili na badala yake langoni alisimama, Beno Kakolanya, kutokana na mlinda mlango huyo kusumbuliwa na malaria pamoja na tumbo.

Akaunti ya mabao ya Simba ilifunguliwa dakika ya 52, wakati Chama alipokokota mpira kwa umbali mrefu, kabla ya kumegea pande Mzambia mwenzake ambaye aligeuka na kumhadaa beki mmoja wa Coastal Union kabla ya kuachia shuti la mguu wa kulia lililojaa wavuni.

Ilikuwa ni dakika moja tu baada ya kukosa bao rahisi zaidi kuliko alilolifunga. Nahodha wa Coastal Union alimfanyia madhambi beki wa kulia Shomari Kapombe na mwamuzi Jonesia akaamuru penalti ambayo kwa mara nyingine tena, Phiri akaukwamisha wavuni dakika ya 60 akimwacha kipa Mcomoro, Mahmoud Mroivili, akiruka bila mafanikio.

Kakolanya alifanya kazi ya ziada dakika ya 67, baada ya kupangua shuti kali la Mcameroon, Bertrand Konfor, kwa mkono wa kushoto na kuiweka salama timu yake.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >